SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI 2022
NA MPANGO WA MAENDELEO 2022/23

KITABU CHA PILI

TUME YA MIPANGO - ZANZIBAR
JUNI, 2022

YALIYOMO:

Mada Ukurasa

YALIYOMO: ..... **i**
Orodha ya Viambatisho iii
1.0 UTANGULIZI **1**
2.0 MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2021 ..... **2**
2.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia 2
2.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika 2
2.3 Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara 3
2.4 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ya Mashariki 3
2.5 Mwelekeo wa Mfumko wa Bei wa Dunia 3
3.0 MWELEKEO WA UCHUMI WA ZANZIBAR 2021 ..... **4**
3.1 Mwelekeo wa Mfumko wa Bei Zanzibar 5
4.0 MIKAKATI YA KISEKTA **6**
5.0 SHABAHA NA MALENGO YA UCHUMI KWA 2021/22-2023/24 ..... **6**
6.0 MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/23 ..... **6**
7.0 MIRADI YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2022/23 ..... **7**
8.0 RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/23 ..... **8**
9.0 MWELEKEO WA PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO NA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2022/23 ..... **9**
9.1 Ofisi ya Rais Ikulu 9
9.2 Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji 11
9.3 Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango 13
9.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar 15
9.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali 18
9.4 Ofisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora 19
9.4.1 Mahakama Kuu 20
9.5 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ 21
9.5.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar 23
9.5.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM) 24

9.5.3 Kikosi cha Valanti 25
9.5.4 Chuo cha Mafunzo 26
9.5.5 Jeshi la Kujenga Uchumi 26
9.5.6 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi 27
9.6 Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais 28
9.6.1 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya ... 30
9.7 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi 31
9.8 Wizara ya Afya 32
9.9 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi 38
9.10 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda 39
9.11 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali 41
9.12 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo 44
9.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo 46
9.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto 50
9.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini 50
9.16 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi 55
9.17 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi 58
9.18 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale 62
10. PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA MFUKO WA MIUNDOMBINU (INFRASTRUCTURE FUND) . 62
11.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI 63
12.0 WASHIRIKA WA MAENDELEO 63
13.0 HITIMISHO 64

Orodha ya Viambatisho

Kiambatisho 1: Mgao wa Fedha za Programu na Miradi ya Maendeleo 2022/23 Kiwizara.
Kiambatisho 2: Programu na Miradi ya Maendeleo Chini ya Mfuko wa Miundombinu (Infrastructure Fund)

1.0 UTANGULIZI

Mikakati na Mipango mbali mbali ya kukuza uchumi na ustawi wa jamii inaendelea kuandaliwa na kutekelezwa ikiwa na azma ya kuinua uchumi, kupunguza umasikini pamoja na kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi. Ili kuweza kupata maendeleo ya kasi ambayo yataambatana na ukuaji uchumi utakaoliwezesha Taifa kufikia malengo na shabaha iliyokusudia, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapanga kutekeleza programu na miradi mbali mbali ya maendeleo itakayoweza kuleta matokeo makubwa na kwa haraka ikiwemo upatikanaji ajira kwa wananchi, kuongeza uwekezaji, kuimarisha hali za wananchi pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Juhudi za kuimarisha Uchumi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali zinaendelea kuleta mafanikio katika Kukuza Uchumi na kuleta maendeleo ya kiuchumi. Kwa mwaka 2022 Uchumi wa Zanzibar unakadiriwa kukua kwa asilimia 5.4 kutoka ukuaji wa asilimia 5.1 ya mwaka 2021.

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/23 utaendelea kuimarisha maeneo ya kukuza uchumi na ustawi wa kijamii kwa ujenzi wa miundombinu ya usafiri, kuimarisha ubora wa elimu, huduma za afya, michezo, upatikanaji wa maji safi na salama na kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa haki za kisheria kwa urahisi na muda mfupi. Mkazo zaidi utawekwa katika kuendeleza miundombinu ya msingi ya barabara, viwanja vya ndege, bandari, ujenzi wa viwanda vya kusarifu samaki na dagaa, mageuzi katika sekta ya nishati (ZESTA) na ukuzaji wa biashara ya kitaifa na kimataifa. Aidha, Mpango utajikita katika kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa za kesi, ujenzi wa mahkama za Mkoa sambamba na kuanza ujenzi wa mji wa Serikali.

Kitabu hiki kinatoa Mwelekeo wa Hali ya Uchumi kwa mwaka 2022 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/23 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025, Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi pamoja na Maelekezo ya Serikali kiujumla. Aidha, ahadi mbali mbali zilizotolewa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi wakati wa kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 na katika ziara za makundi mbali mbali pamoja na miongozo iliyotolewa na viongozi wakuu kupitia sekta tofauti nayo pia imezingatiwa inavyostahiki.

2.0 MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI KWA MWAKA 2021

2.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia.

Wakati vita ya Urusi ikiendelea nchini Ukraine athari zake na hasa kiuchumi zinaendelea kujitokeza katika sehemu mbalimbali za ulimwengu na barani Afrika ni moja ya eneo zinakoshuhudiwa athari kadhaa. Mataifa mbali mbali duniani yameshatahadharisha kwamba vita hivyo vinavyoendelea vitasababisha ongezeko la bei ya bidhaa nchini humo na kuzorotesha shughuli za maendeleo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha Duniani (IMF) makadirio ya ukuaji wa uchumi ni kufikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2022 kinyume na matarajio ya awali ya ukuaji wa asilimia 4.4 kutoka asilimia 6.1 iliyoripotiwa mwaka 2021.

Kwa Nchi Zilizoendelea kasi ya ukuaji inatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2022, kinyume na matarajio ya awali ya ukuaji wa asilimia 4.0 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2021. Uchumi wa Umoja wa Ulaya unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2022 matarajio ya awali ni kukua na kufikia asilimia 3.9 kutoka ukuaji wa asilimia 5.3 mwaka 2021. Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi kasi ya ukuaji inatarajiwa kufikia asilimia 3.8 mwaka 2022 kinyume na matarajio ya awali ya ukuaji wa asilimia 4.8 kutoka ukuaji wa asilimia 6.8 mwaka 2021. Kwa upande wa Nchi za Afrika Mashariki uchumi unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2022 kutoka ukuaji wa asilimia 4.1 mwaka 2021.

Pamoja na udhibiti wa maambukizi mapya ya ugonjwa wa UVIKO-19 mwelekeo wa uchumi duniani umekuwa hauna uhakika kutokana na vita vya Mashariki ya Ulaya ingawa tayari mazungumzo ya kumaliza mgogoro wa Urusi na Ukraine yanaendelea.

2.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika

Kwa makadirio ya awali kwa mwaka 2022, kasi ya ukuaji wa uchumi Barani Afrika inatarajiwa kupanda na kufikia wastani wa asilimia 4.0 kutoka wastani wa asilimia 3.4 iliyorikodiwa mwaka 2021. Ukuaji wa mwaka 2022 utatokana na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi ikiwemo uzalishaji wa mafuta na kuongezeka kwa uchimbaji wa madini pamoja na kuongezeka kwa bei za bidhaa kwa mauzo ya nje ya nchi.

2.3 Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara

Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa sehemu kubwa zinatekeleza dhana ya biashara huria na ni ukanda wenye watu wengi sana wanaokadiriwa kufikia watu 1.2 bilioni. Kupunguwa kwa maambukizi ya Ugonjwa wa COVID 19 kumesababisha kuongezeka kwa uzalishaji viwandani na kuongezeka uwekezaji. Kasi ya ukuaji uchumi katika ukanda huo inategemewa kuimarika kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2021. Hata hivyo, makadirio ya ukuaji wa uchumi yatafikiwa ikiwa migogoro na vita vinavyoendelea baina ya Urusi na Ukraine vitamalizika.

2.4 Mwelekeo wa Uchumi wa Afrika ya Mashariki

Makadirio ya awali, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki mwaka 2022 inatarajiwa kuimarika kutokana na kuimarika kwa shughuli za viwanda, sekta ya huduma na sekta ya kilimo hususani katika nchi ya Tanzania, Rwanda na Uganda. Ukuaji wa uchumi unatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 5.8 kwa mwaka 2022 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.1 ya mwaka 2021.

Uchumi wa nchi ya Uganda unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.0 kwa mwaka 2022 kutoka asilimia 3.4 mwaka 2021, Kenya unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2022 kutoka asilimia 5.6 mwaka 2021. Tanzania kukua kwa wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2022 kutoka asilimia 4.9 mwaka 2021. Rwanda unatarajiwa kukua na kufikia wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2022 kutoka asilimia 10.2 mwaka 2021 na nchi ya Burundi uchumi unatarajiwa kukua na kufikia wastani wa asilimia 2.1 kwa mwaka 2022 kutoka asilimia 2.0 mwaka 2021.

2.5 Mwelekeo wa Mfumko wa Bei wa Dunia

Mfumko wa bei duniani unatarajiwa kupanda kufuatia vita vya Ukraine na Urusi, mijadala imejikita katika kupunguza kasi na ukubwa wa mfumko wa bei duniani. Hali hii imeathiri zaidi kampuni zinazotaka kukopa fedha za kuwekeza, Serikali zinazotaka kufadhili matumizi ya umma, na pia kuathiri watu wanaohitaji mikopo ya kununua nyumba, gari au kufadhili gharama zisizotarajiwa kwa wananchi. Kinyume cha matarajio ya awali kasi ya mfumko wa bei wa Dunia inatarajiwa kufikia wasatani wa asilimia 6.0 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2021.

Kwa Nchi Zilizoendelea kasi ya mfumko wa bei inatarajiwa kupanda na kufikia wastani wa asilimia 3.9 kwa mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2020. Kutokana na kupanda kwa bei za nishati, gesi, sukari na ngano kutokana na athari ya vita vya Ukraine na Urusi kwa vile nchi hizo ni wazalishaji wakubwa wa bidhaa hizo duniani. Aidha, Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi mfumko wa bei unatarajiwa kupanda na kufikia wastani wa asilimia 5.9 kwa mwaka 2022 kutoka wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2020.

3.0 MWELEKEO WA UCHUMI WA ZANZIBAR 2021

Mwelekeo wa hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2022 ni kwa mujibu wa viashiria vya uchumi jumuishi na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar kwa Mwaka 2022/23 na kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali vilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050. Kwa mwaka 2022 Uchumi wa Zanzibar unategemewa kukua kwa asilimia 6.8 kutoka ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2021. Ukuaji huo utatokana na mambo yafuatayo:-

i. Kupatikana kwa fedha za mkopo nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) na mkopo maalum kutoka Benki Kuu ya Tanzania;

ii. Kuendelea kuongezeka kwa uingiaji wa watalii na kukadiriwa kufikia watalii 450,213 kwa mwaka 2022 ikiwa hali ya dunia itaendelea kuwa salama bila ya migogoro. Matarajio ya kuongezeka kwa watalii hapa Zanzibar, yanachangiwa na dalili zilizoanza kuonekana mara baada ya Uzinduzi wa Filamu ya Tanzania, ***The Royal Tour*** ambayo imeshirikisha viongozi wetu wakuu wa nchi ambao ni Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

iii. Matarajio ya kuongezeka kwa mapato ya ndani kwa asilimia saba (7%) kutokana na utekelezaji wa mikakati inayofanywa na Serikali ikiwemo matumizi ya mifumo ya kielekroniki kwa ukusanyaji wa mapato na kuondoa misamaha ya kodi isiyo na tija;

iv. Kuongezeka kwa uwekezaji na uzalishaji viwandani, ikiwemo uwekezaji mkubwa kwenye visiwa vidogo vidogo, uzalishaji wa nguo kutoka kiwanda cha Basra, kiwanda cha maji Chamanangwe na kiwanda cha viatu cha Amani. Matarajio ya uwekezaji pia katika

maeneo mengine mengi, ikiwemo uwekaji wa mawe ya msingi, ufunguzi na kuanza kazi kwa Hoteli za Kitalii za madaraja mbali mbali zikiwemo Hoteli ya Marijani, Riu, Palolo na L'oasis ambazo zitasaidia katika kutoa huduma za kitalii na kuzalisha ajira hapa nchini.

v. Kuimarika kwa shughuli za kibiashara hasa kwa wajasiriamali wadogo wadogo baada ya kupatikana wa fedha za mkopo nafuu;

vi. Kudhibiti kwa matumizi ya Serikali kupitia kuimarika kwa mifumo ya mapato na matumizi ya kibajeti ikiwemo mfumo wa BAMAS na kuelekeza matumizi hayo katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

vii. Kuimarika kwa huduma za abiria na mizigo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amaan Karume ambako kutawezesha kuhudumia ndege za kubwa za kimaitafa zinazofika Zanzibar kwa viwango cha kimataifa.

Hata hivyo, kutokana na kuibuka kwa vita vya Urusi na Ukraine vinavyoendelea kumepelekea athari kubwa za kiuchumi duniani kote. Kwa upande wa Zanzibar athari zinazotarajiwa kujitokeza ni pamoja na:-

i. Kupungua kwa sekta ndogo za Uzalishaji na Usafirishaji wa Bidhaa kutokana na kupanda kwa bei za nishati ya mafuta;

ii. Ongezeko la bei za bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula;

iii. Matumizi makubwa ya fedha za kigeni za kuagiza bidhaa nje ya nchi ikiwemo nishati ya mafuta, hali hii inaathiri akiba ya fedha za kigeni ya nchi na kupunguza matumizi ya fedha hizo;

iv. Hofu ya kupungua kwa Watalii kutoka nchi za Urusi na Ukraine ambapo kwa miaka ya karibuni watalii kutoka nchi hizo waliongezeka. Kwa mwaka 2021 walifikia 85,196 sawa na asilimia 21.5 ya watalii wote walioitembela Zanzibar.

Kufuatia hali hii, Zanzibar inatarajiwa kuendelea kuathirika kiuchumi na matarajio mapya ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2022 ni kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 5.4 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2021.

3.1 Mwelekeo wa Mfumko wa Bei Zanzibar

Makadirio ya hali ya mfumko wa bei wa Zanzibar yanaonesha kuwa mfumko wa bei wa Zanzibar utapanda kutokana na migogoro na vita vinavyoendelea Mashariki ya Ulaya. Hiyo inatokana na kuwa zaidi ya asilimia 50 ya bidhaa

zinazotumika Zanzibar zinatoka nje ya nchi, ambapo kwa sasa dunia imethibitisha hali ya mfumko wa bei kwa bidhaa muhimu kwa matumizi ya kawaida. Hata hivyo, juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuhakikisha bei za bidhaa na huduma hazipandi kwa kuweka mikakati ya kuzuwia kupanda kwa bei. Kwa mwaka 2022 kasi ya mfumko wa bei inatarajiwa kuwa zaidi ya asilimia 5 kinyume cha matarajio ya awali.

4.0 MIKAKATI YA KISEKTA

Kwa mwaka 2022, mkazo utawekwa katika maeneo yafuatayo:-

i. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu;
ii. Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu;
iii. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi;
iv. Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii; na
v. Utawala Bora na Uhimili.

5.0 SHABAHA NA MALENGO YA UCHUMI KWA 2022/23

Malengo na Shabaha za Uchumi Jumuishi kwa Mwaka 2022/2023katika kipindi cha mwaka 2022/2023, shabaha za uchumi jumuishi zilizozingatiwa katika Mpango ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2022;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei na kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 24.7 ya Pato la Taifa mwaka 2022/2023 kutoka wastani wa asilimia 19.6 ya mwaka 2021/2022;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 18.1 ya Pato la Taifa mwaka 2022/2023 kutoka asilimia 15.8 mwaka 2021/2022; na

(v) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa chini ya asilimia 3.0 ya Pato la Taifa ili kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

6.0 MWELEKEO WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/23

Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/23 ni mwendelezo wa utekelezaji wa malengo na mikakati inayotokana na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 yenye lengo la kuifikisha Zanzibar katika nchi ya Kiwango

cha Juu cha Uchumi wa Kati (Upper Middle-Income Status) kupitia mihimili mikuu minne ambayo ni Mageuzi ya kiuchumi; Maendeleo ya rasilimali watu na huduma za kijamii; Kuimarisha miundombinu; na Utawala bora na uhimili.

Licha ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050, Mpango huu pia umezingatia Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi, Maelekezo ya Serikali kiujumla pamoja na ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa wananchi wakati wa Kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na ziara za makundi mbali mbali pamoja na miongozo iliyotolewa kwa viongozi wakuu kupitia sekta tofauti.

Katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa pogramu na miradi ya maendeleo imepangwa kutekelezwa ili kuweza kuifikisha Zanzibar sehemu iliyokusudiwa. Kwa mwaka 2022/23, Mpango wa Maendeleo umezingatia utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo inayojikita katika kuimarisha hali za wananchi, kuongeza uwekezaji, kuongeza uwezo wa rasilimali watu, kukuza ajira na hatimae kuongeza mapato ya Serikali ili kuwezesha kuleta matokeo ya haraka katika kuhakikisha huduma muhimu zinapatikana kwa viwango stahiki pamoja na kukuza shughuli za kiuchumi.

7.0 MIRADI YA KIMKAKATI KWA MWAKA 2022/23

Katika Mpango wa Maendeleo wa 2022/23 Serikali imedhamiria kutekeleza miradi maalum ya kimkakati katika maeneo mahsusi yenye lengo la kuimarisha Ukuzaji wa Uchumi, miundombinu, huduma za jamii na utawala bora. Maeneo haya ni yale ambayo yanatarajiwa kuleta matokeo makubwa na kwa haraka ikiwemo upatikanaji ajira nyingi kwa wananchi, kuongeza uwekezaji, kuimarisha hali za wananchi pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Kwa kuzingatia maeneo hayo, programu na miradi ya kimkakati inayotarajiwa kutekelezwa ni kama ifuatayo:-

i. Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu

a) Ujenzi wa bandari za kisasa za uvuvi; na

b) Ujenzi wa viwanda vya kutengeneza maboti na kusarifu samaki na dagaa.

ii. Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu

a) Ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Karume - Pemba;

b) Ujenzi wa barabara kuu (km 125.6) na barabara za ndani (km 275.9);

c) Matengenezo ya barabara za mjini(km 103.7);

d) Ujenzi wa Bandari jumuishi ya Mangapwani; na

e) Kuifanyia mabadiliko sekta ya nishati.

iii. Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi

a) Kuendeleza kituo cha biashara na maonesho ya Kimataifa Zanzibar-Nyamanzi.

iv. Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii

a) Uimarishaji wa viwanja vya michezo vya Wilaya; na

b) Ujenzi wa vituo vya amali kwa kila Wilaya.

v. Utawala Bora na Uhimilivu

a) Ujenzi wa Mahkama za Mikoa;

b) Kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa taarifa za kesi (ECMIS); na

c) Ujenzi wa Mji wa Serikali.

8.0 RASILIMALI KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2022/23

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/23 unalenga kutekeleza jumla ya programu 29 (program nne ni mpya) na miradi 43 (miradi 16 ni mipya) ya maendeleo. Programu mpya zitakazotekelezwa ni (i) Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Uvuvi; (ii) Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia; (iii) Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani; na (iv) Programu ya Matengenezo ya Barabara za mjini. Kwa upande wa miradi mipya itakayotekelezwa ni (i) Uimarishaji Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais; (ii) Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi; (iii) Uratibu wa Shughuli za Kupambana na Umasikini; (iv) Ujenzi wa Mahkama za Mikoa; (v) Uanzishwaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Kesi (ECMIS); (vi) Uimarishaji wa Mifumo ya Taka na Maji Taka Zanzibar; (vii)

Kuimarisha Uzalishaji wa Idara Maalum za SMZ; (viii) Kuanzisha Bima ya Afya Zanzibar; (ix) Kuwekeza katika huduma za Mama na Mtoto; (x) Matengenezo ya Nyumba za Maendeleo; (xi) Utayarishaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi; (xii) Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa; (xiii) Uanzishwa wa Viwanda vya Maboti, Kusarifu Dagaa na Samaki; (xiv) Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini; (xv) Ujenzi wa Bandari za Kisasa za Uvuvi; na (xvi) Maendeleo ya Uchumi wa Buluu.

Kwa mwaka 2022/23 Mpango wa Maendeleo umetengewa jumla ya TZS 1,352.19 bilioni kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo ikiwa ni ongezeko la TZS 469.65 bilioni sawa na asilimia 53.20 ikilinganishwa na Bajeti ya Maendeleo ya mwaka 2021/22 ya TZS 882.5 bilioni. Kati ya fedha hizo za Maendeleo (TZS 1,352.19 bilioni), TZS 748.2 bilioni ni kwa programu na miradi ya maendeleo ya kimkakati na TZS 603.9 bilioni ni kwa programu na miradi mengineyo. Serikali imepanga kutumika jumla ya TZS 682.54 bilioni sawa na asilimia 50.47 ya Bajeti ya Maendeleo. Aidha, jumla ya TZS 669.65 bilioni sawa na asilimia 49.53 ya bajeti ya maendeleo zimepangwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 62.78 bilioni ni ruzuku na TZS 606.86 bilioni ni mikopo. Fedha hizo ni ongezeko la TZS 393.31 bilioni sawa na asilimia 142.34 ikilinganishwa na fedha zilizotengwa kwa mwaka 2021/22 zenye jumla ya TZS 276.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kugharamia programu na miradi ya maendeleo.
Mgawanyo wa makisio ya fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo kiwizara kwa programu na miradi ya maendeleo unaonekana kwenye kiambatisho namba 1.

9.0 MWELEKEO WA PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO NA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA 2022/23

9.1 Ofisi ya Rais Ikulu

Ofisi ya Raisi Ikulu ina jukumu la kusimamia shughuli za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi sambamba na kusimamia shughuli za Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi (Diaspora). Ofisi hii pia ina wajibu wa kuhakikisha jamii inapata habari juu ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo na sera zinazotekelezwa na Mheshimiwa Rais wa

Zanzibar ili kukuza uelewa kwa wananchi juu ya utekelezaji wa mipango ya nchi. Kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 4.0 bilioni kutoka Serikalini.

Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali

Mradi umeanzishwa mwaka 2009/20 ukiwa na lengo la kuimarisha maakazi ya viongozi wakuu wa nchi na kuweka mandhari na mazingira mazuri ya makaazi hayo. Mradi huu ni wa Awamu ya Pili na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025 ukiwa na makadirio ya gharama za TZS 10.0 bilioni. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 2.4 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa kutekelezwa

i. Ujenzi wa Ikulu ndogo ya Bwefum - Unguja na Minyenyeni, Wete - Pemba; na

ii. Ununuzi wa samani za Ofisi.

Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais

Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais umeanzishwa mwaka 2022/23 na unatarajiwa kukamilika 2024/25. Lengo la mradi ni kuimarisha mfumo wa ulinzi na usalama katika majengo ya Ikulu pamoja na makaazi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili kuwa na miundombinu imara na endelevu inayokwenda na wakati. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.6 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa

i. Uimarishaji wa Sera ya TEHAMA na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Raisi;

ii. Ufungaji wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya uimarishaji wa mfumo mtandao kwa maeneo ya Ikulu;

iii. Kutoa mafunzo yanayohusiana na TEHAMA (ICT) kwa watumishi; na

iv. Ufungaji wa vifaa kwa ajili ya kuhuwisha nyaraka na kuzihifadhi kwa kutumia mbinu za kisasa.

9.2 Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji

Ofisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji inasimamia Idara na Taasisi ambazo zina jukumu la kutekeleza malengo ya Wizara ikiwa ni pamoja na kusimamia upatikanaji wa kazi za staha na kuzingatia sheria na viwango vya kazi, kuimarisha hali ya kijamii na kiuchumi ya wananchi wa Zanzibar, kuimarisha na kukuza uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na kukuza na kusimamia uwekezaji kwa maendeleo ya nchi. Aidha, Wizara hii inatekeleza shughuli zake kupitia mipango na mikakati ya kimaendeleo ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja na mradi mmoja wa maendeleo kwa jumla ya TZS 42.7 bilioni kutoka Serikalini.

Programu ya Kuimarisha Uwezeshaji Wananchi Zanzibar

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kutoa fursa za ajira kwa kuweka mazingira bora na kuwajengea uwezo vijana na wanawake ili kupunguza umaskini Zanzibar. Kwa mwaka 2022/23, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 27.6 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi mitatu kama ifuatavyo:-

Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Kulea na Kukuza Wajasiriamali

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2021/22 kwa lengo la kukuza na kuimarisha shughuli za ujasiriamali kwa wananchi wa Zanzibar sambamba na kupunguza umaskini. Mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 19.9 bilioni hadi kukamilika kwake mwaka 2023/24 na kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 15.0 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kujenga vituo vya kulea na kukuza wajasiriamali Tunguu – Unguja na Mbuzini – Pemba.

Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Kutoa Huduma za Ujasiriamali na Biashara (EBDS)

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha masoko na bidhaa za wajasiriamali sambamba na kuhakikisha huduma za wajasiriamali zinapatikana kwa ufanisi zaidi. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.5 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa vituo katika Mkoa wa Kusini Pemba, Kusini na Kaskazini Unguja; na

ii. Ununuzi wa vifaa.

Mradi wa Ujenzi wa Vituo Jumuishi vya Wajasiriamali

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2022/23 ukiwa umelenga kuanzisha kituo cha uchakataji cha pamoja chenye kutoa huduma zote zinazohitajika katika usindikaji wa mazao mbali mbali yakiwemo ya kilimo, vipodozi na utengenezaji wa nguo ili kuondoa changamoto zinazowakabili wafanyabiashara wakubwa na wa kati Zanzibar. Kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 8.1 bilioni zimepangwa kutumika.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa vituo viwili vya kutoa huduma jumuishi Unguja na Pemba; na

ii. Ununuzi wa vifaa na samani.

Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2021/22 ukiwa na lengo la kuimarisha miundombinu wezeshi ya kuvutia uwekezaji ikiwemo barabara, maji na umeme ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi na hivyo kuimarisha sekta ya uwekezaji nchini. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021 - 2025). Kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 15.1 bilioni zimepangwa kutumika.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa barabara za ndani eneo la uwekezaji la Micheweni na Fumba; na

ii. Kuweka miundombinu ya maji na umeme eneo la uwekezaji la Micheweni.

9.3 Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango

Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ina jukumu la kusimamia shughuli zote zinazohusiana na maendeleo ya fedha, uchumi na mipango kitaifa. Miongoni mwa shughuli hizo ni kusimamia mapato na matumizi, mali za Serikali, mipango ya kitaifa, kikanda na kimataifa, usimamizi wa uchumi mkuu pamoja na shughuli zote za Taasisi nyengine zinazohusiana na masuala ya fedha na mipango nchini. Aidha, Ofisi hii huishauri Serikali katika masuala ya kifedha na kiuchumi, kutayarisha bajeti ya Serikali na kusimamia utekelezaji wake, kutunga sheria na sera za fedha na kodi, kupanga mafungu ya matumizi ya fedha kwa taasisi mbali mbali za Serikali. Kwa mwaka 2022/23, Ofisi hii imepangiwa jumla ya TZS 143.45 bilioni (TZS 92.20 bilioni kutoka Serikalini na TZS 51.25 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kuteleza programu tatu na mradi mmoja wa maendeleo.

Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar

Programu hii ina jukumu la kusimamia ujenzi wa Ofisi za Serikali katika maeneo ambayo yamependekezwa na Serikali kwa ajili ya kuweka mazingira bora ya kazi kwa wafanyakazi wa Serikali. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa jumla ya TZS 92.20 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ukamilishaji wa kazi ya utanuzi na ujenzi wa Ofisi za Serikali ikiwemo: Skuli ya Sheria, Ofisi ya Mufti, Nyumba ya Makamo wa Kwanza wa Rais, Nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais, Ofisi ya Shirika la Magazeti, Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo na vya Kati (SMIDA); na

ii. Kuanza ujenzi wa Mji wa Serikali.

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar inalenga kuimarisha miundombinu na huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Programu hii itatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021/26) kwa gharama za jumla ya TZS 346.5 bilioni. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 47.13 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua na barabara za ndani kwa maeneo ya Sebleni – Kwawazee, Meya-Magomeni na Tomondo;

ii. Ununuzi wa vifaa vya usafi (magari ya taka, makontena ya kuwekea taka na gari la kusafishia barabara) kwa Mabaraza ya Miji na Manispaa Unguja na Pemba;

iii. Kufanya upembuzi yakinifu wa uendelezaji wa urithi wa kihistoria ya Mji Mkongwe (Green Corridor);

iv. Ununuzi wa vifaa vya uchunguzi vya maabara ya Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS); na

v. Kuzijengea uwezo Taasisi za Serikali zinazosimamia maendeleo ya Miji, ikiwemo kuwapatia mafunzo ya muda mfupi watendaji wa Taasisi hizo pamoja na ununuzi wa vitendea kazi.

Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP – V)

Programu ina lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Programu imeanzishwa mwaka 2017/18 na imekadiriwa kutumia jumla ya TZS 8.80 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa TZS 2.66 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuimarisha miundombinu ya mfumo wa TEHAMA wa Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB);

ii. Kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa kutoza ushuru;

iii. Kuendeleza mfumo wa usimamizi wa fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo;

iv. Kuandaa Mkakati wa Kusimamia Madeni ya Umma;

v. Kukamilisha Sheria ya Bajeti;

vi. Kuandaa mwongozo wa usimamizi wa mikataba;

vii. Kuimarisha uendeshaji wa Idara ya Usajili wa Hazina;

viii. Kuandaa Mfumo na Mwongozo wa Usimamizi wa Fedha za Serikali; na

ix. Kuandaa Sheria ya Ukaguzi wa Ndani.

Mradi wa Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili
Mradi una lengo la kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili. Mradi umeanza mwaka 2016/17 na umekadiriwa kutumia jumla ya TZS 6.20 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2022/23, mradi huu umepangiwa TZS 1.46 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuandaa Sheria ya Madini ya Zanzibar na Kanuni zake;
ii. Kuandaa Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Petroli (PRMA) pamoja na Kanuni za GFS za Mafuta na Gesi; na
iii. Kuandaa Sheria ya Ushuru wa Mafuta ya Petroli na Ushuru wa Faida ya Ziada.

9.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar

Tume ya Mipango ina jukumu la kupanga, kuratibu na kusimamia mipango ya kiuchumi na kijamii Zanzibar ikiwemo mipango ya maendeleo ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi, maeneo ya kipaumbele ya tafiti mbali mbali, pamoja na masuala ya idadi ya watu na miradi ya maendeleo. Aidha, Tume inashughulikia uratibu na upangaji wa vipaumbele vya Taifa sambamba na kutoa miongozo na kusimamia masuala ya Uchumi Mkuu wa nchi na kufanya ufuatiliaji na tathmini wa mipango na miradi ya maendeleo. Kwa mwaka 2022/23, Tume ya Mipango imepanga kutekeleza programu moja na miradi mitatu ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 12.81 bilioni (TZS 12.08 bilioni kutoka Serikali na TZS 730 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Programu ya Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)
Programu hii imelenga kuwakwamua wananchi na umasikini kupitia urasimishaji wa ardhi na biashara ili ziweze kutumika katika juhudi za kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Utekelezaji wa MKURABITA ulianza rasmi 2008/09 kwa upande wa Zanzibar ukiwa na lengo la kuwawezesha wananchi wanaomiliki rasilimali na kuendesha biashara nje ya mfumo usio rasmi waweze kuzirasimisha, kuzitumia na kupata mitaji kwa ajili ya kushiriki katika uchumi wa kisasa ulio rasmi. Kwa mwaka 2022/23, programu imepanga kutumia kiasi cha TZS 4.50 bilioni (TZS 4.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 500 milioni kutoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali (SMZ)

i. Kutayarisha na kuchapisha hati za usajili kwa maeneo yaliyotambuliwa;
ii. Kufanya utambuzi wa ardhi katika maeneo ya Shakani, Mbweni, Mombasa kwa Mchina, Kidoti, Mahonda, Uroa, Fuoni na Amani kwa upande wa Unguja na Bopwe, Utaani na Micheweni kwa upande wa Pemba;
iii. Kutoa mafunzo na kuwahakiki wafanyabiashara wadogo wadogo 150 kwa kila Wilaya Unguja na Pemba;
iv. Kuanzisha vituo jumuishi vitano vya urasimishaji biashara, vitatu Unguja (Wilaya ya Kaskazini 'B', Kati na Magharibi 'A') na viwili Pemba (Wilaya ya Wete na Mkoani);
v. Ununuzi wa GPS mbili na vitendea kazi vya Ofisi;
vi. Kuratibu vikao viwili vya kamati kiongozi na vikao vinne vya kamati ya wataalamu; na
vii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za MKURABITA.

Shughuli zilizopangwa kuekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

i. Kuanzisha vituo jumuishi viwili vya urasimishaji biashara (Wilaya ya Kusini Unguja na Micheweni Pemba);
ii. Ujenzi wa masjala ya ardhi Unguja;
iii. Kutoa elimu ya uhamasishaji na kushiriki maonyesho mbali mbali; na
iv. Ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za mradi.

Uratibu wa Shughuli za Kupambana na Umasikini

Mradi wa Uratibu wa Shughuli za Kupambana na Umasikini umeanzishwa kwa lengo la kusaidia Serikali katika jitihada zake za kupunguza umasikini Zanzibar. Mradi huu umejikita katika kuainisha sababu zinazopelekea kuwepo kwa umasikini zaidi katika baadhi ya maeneo, kutoa elimu na kuandaa mikakati ya kupunguza umasikini. Mradi huu unatekelezwa na Serikali ambapo kwa mwaka 2022/23 umepangiwa jumla ya TZS 800 milioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kufanya utafiti wa hali ya umaskini kwa shehia zilizoainishwa katika ripoti ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS) ya 2019/20;

ii. Kuandaa mfumo wa usimamizi wa taarifa kwa maeneo maskini;
iii. Kufanya uratibu na kusimamia shughuli za umasikini kwa wadau wa kupunguza umaskini;
iv. Kuwajengea uwezo watendaji juu ya kuandaa mikakati ya kupunguza umasikini; na
v. Kuandaa maadhimisho ya wiki ya kupambana na umasikini Duniani.

Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi

Mradi wa Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi una lengo la kuimarisha uandaaji na utayarishaji wa ripoti za upembuzi yakinifu kwa program na miradi ya maendeleo. Mradi huu kwa awamu ya kwanza utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (2022/23-2024/25) na utagharimu jumla ya TZS 23.4 bilioni. Aidha, mradi huu utasaidia kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutoa taarifa za kitaalamu zinazoainisha hali halisi ya uwezekano wa utekelezaji wa mradi na tija ambayo inaweza kupatikana kwa kutekeleza mradi huo na kuainisha mbinu za maeneo ya kuimarisha utekelezaji wenye kuleta ufanisi katika miradi ya maendeleo. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 6.98 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kufanya upembuzi yakinifu kwa programu/miradi ya maendeleo;
ii. Kuandaa mfumo wa ukusanyaji taarifa na ripoti za upembuzi yakinifu kwa programu/miradi ya maendeleo; na
iii. Kujenga uwezo wa Taasisi na watendaji juu ya utayarishaji na uchambuzi wa ripoti za upembuzi yakinifu kwa programu na miradi ya maendeleo.

Mradi wa Usimamizi, Kujenga Uwezo na Kuoanisha Mipango ya Kisekta, Kitaifa na Kimataifa

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha usimamizi na kuoanisha mipango ya kisekta, kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Malengo ya Maendeleo ya Afrika (African Agenda 2063). Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa jumla ya TZS 530 milioni (TZS 300 milioni kutoka Serikalini na TZS 230 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo)

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali

i. Kuandaa mpango wa utekelezaji wa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini;
ii. Kuandaa ripoti ya mwaka ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP); na
iii. Kutoa uwelewa kwa wadau kuhusiana na Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini.

Shughuli zilizopangwa kuekelezwa na Washirika wa Maendeleo

i. Kushiriki mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa; na
ii. Kufanya maandalizi ya Ripoti ya Utekelezaji wa Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063, kwa upande wa Zanzibar kwa mwaka 2023/24.

9.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Ofisi ina jukumu la kuratibu uzalishaji, ukusanyaji, uchambuzi, uchapishaji, uhifadhi na usambazaji wa taarifa na takwimu zilizo rasmi, kutoa takwimu na taarifa zenye ubora na kuhamasisha matumizi ya takwimu katika mipango ya maendeleo, kufanya maamuzi katika masuala ya utawala na uendeshaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kutekeleza mradi mmoja wenye jumla ya TZS 13.26 bilioni. Kati ya fedha hizo TZS 500 milioni kutoka Serikalini na TZS 12.7 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mradi wa Uendelezaji Takwimu Zanzibar (ZSDP)

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji na usimamiaji wa takwimu sahihi katika mfumo wa takwimu Zanzibar ambazo zitatumika kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini mipango ya maendeleo ya kisekta, kitaifa, kikanda na kimataifa. Kwa mwaka 2022/23, Mradi umepangiwa jumla ya TZS 13.2 bilioni, kati ya fedha hizo TZS 500 milion ni kutoka Serikalini na TZS 12.7 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali

i. Ujenzi wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali - Pemba

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Washirika wa Maendeleo

i. Kufanya Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2022;
ii. Utekelezaji wa Mpango wa Uimarishaji Takwimu Tanzania (TSMP-II);

iii. Kuratibu upatikanaji wa viashiria vya jinsia;

iv. Kuimarisha mfumo wa Taifa wa Takwimu za Idadi ya Watu; na

v. Kufanya Utafiti wa Viashiria vya Ukimwi.

9.4 Ofisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

Ofisi ina lengo la kuwa na utumishi wa umma ulio bora kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa jamii kwa kuzingatia misingi ya haki, Sheria, demokrasia na utawala bora ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma nzuri kwa wananchi. Aidha, Ofisi inasimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za sekta ya Sheria, utumishi na utawala bora Zanzibar. Kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kutekeleza programu mbili za maendeleo kwa gharama ya TZS 1.68 bilioni kutoka Serikalini.

Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma kwa Awamu ya II (ZPSRP II)

Programu ina lengo la kukuza uwajibikaji na utendaji kwa watumishi wa umma Zanzibar, kwa kuzingatia taratibu zote za mifumo iliyobora katika utoaji wa huduma kwa ufanisi. Programu imeanza mwaka 2018/19 na imekadiriwa kutumia jumla ya TZS 12.1 bilioni hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa jumla ya TZS 528 milioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuanzisha programu za urahisishaji wa upatikanaji wa huduma katika utumishi wa umma;

ii. Kuendesha mafunzo kwa viongozi katika utumishi wa umma;

iii. Kufanya mapitio ya nyaraka ya Mkakati wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma wa awamu ya pili;

iv. Kuandaa mfumo wa maombi ya ajira kwa njia ya kielektroniki;

v. Kufanya mapitio ya muundo wa utumishi na mfumo wa upandishaji vyeo na madaraja kwa watumishi wa umma;

vi. Kufanya ukaguzi wa watumishi, malipo ya mishahara na stahiki za watumishi; na

vii. Kufanya mapitio ya programu za mafunzo na mitaala ya Chuo cha Utumishi wa Umma.

Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria

Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria imeanzishwa mwaka 2022/23 kwa lengo la kuwezesha wananchi kisheria na kuhakikisha upatikanaji wa haki. Programu hii imepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano 2022/23 hadi 2026/27 na utagharimu jumla ya TZS 5.0 bilioni. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa kiasi cha TZS 1.15 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa

i. Kufanya mapitio ya Sheria zenye mnasaba na Uchumi wa Buluu, Sheria ya Ardhi na Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai;
ii. Kufanya mapitio ya Mkakati wa Haki za Watoto wa mwaka 2013;
iii. Kutafsiri Sheria za Uchumi kwa lugha nyepesi;
iv. Kufanya tathmini ya Sheria za Zanzibar pamoja na utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
v. Kufanya utafiti wa kuangalia mtazamo wa wananchi katika utekelezaji wa sheria Zanzibar;
vi. Kuimarisha uratibu wa utoaji wa huduma za msaada wa kisheria; na
vii. Kuanzisha jukwaa la Sekta ya Sheria.

9.4.1 Mahakama Kuu

Ofisi ina lengo la kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yote ya jinai na madai ya wananchi yanayowasilishwa mahakamani ili kufanikisha upatikanaji wa haki nchini. Kwa mwaka 2022/23, Mahakama imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo yenye jumla ya TZS 6.55 bilioni kutoka Serikalini.

Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi

Mradi umeanzishwa mwaka 2022/23 kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa uendeshaji wa kesi kwa njia ya kielektroniki ambao utaimarisha utendaji wa kazi za mahakama katika kutoa huduma na haki kwa wananchi kwa wakati. Mradi umepangwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili 2022/24 na utagharimu jumla ya TZS 2.1 bilioni. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa mwaka 2022/23

i. Kuimarisha miundombinu katika majengo ya mahakama; na

ii. Kuongeza huduma za kimtandao katika ngazi zote za mahakama.

Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Mikoa

Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Mikoa una lengo la kujenga majengo ya mahakama za Mikoa na Wilaya kwa ajili ya kuimarisha mazingira ya kazi na kuwa na Ofisi za kisasa zitakozoengeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria na upatikanaji wa haki. Mradi huu wa miaka mitano (2022-2027) umepangwa kuanza kutekelezwa mwaka 2022/23 na utagharimu jumla ya TZS 48.6 bilioni. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 5.55 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa

i. Ujenzi wa mahakama ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja;

ii. Ujenzi wa mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Unguja; na

iii. Ujenzi wa mahakama ya Mkoa wa Kusini Pemba

9.5 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Ofisi ina jukumu la kuhakikisha uwepo wa amani na ulinzi shirikishi wa raia na mali zao, kutekeleza kazi za Serikali za Mitaa katika maeneo na mikoa husika, kusimamia mipango ya maendeleo na miongozo ya Serikali. Ofisi hii ndio inayosimamia utekelezaji wa Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ili kuhakikisha zinatekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 18.92 bilioni zilizopangwa kutolewa na Serikali.

Mradi wa Uwekaji wa Kamera na Vifaa vya Ulinzi (Zanzibar Salama)

Mradi wa Zanzibar Salama awamu ya pili umeanzishwa mwaka 2020/21 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2022/23 ambao unagharimu jumla ya TZS 24.77 bilioni. Mradi lengo la kuimarisha ulinzi katika maeneo yote ili kuweka mazingira salama kwa wananchi na wageni katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2022/23, umepangiwa kiasi cha TZS 7.4 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuendelea na kazi za uwekaji wa kamera na vifaa vya ulinzi na usalama katika maeneo ya Wilaya ya Magharibi 'A' na 'B' kwa Unguja, Chake -Chake, Mkoani na Wete kwa Pemba;

ii. Kujenga vituo vya kupokea na kufuatilia taarifa za matukio katika maeneo ya Mkoani, Chake -Chake na Wete kwa Pemba pamoja na ukarabati wa kituo kikuu cha taarifa Unguja;

iii. Kufanya matengenezo ya mifumo na vifaa vya mradi;

iv. Ununuzi wa vitendea kazi vya mradi;

v. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa mradi; na

vi. Kufanya shughuli za uendeshaji na utawala za mradi.

Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Maji Taka Zanzibar

Mradi umeanzishwa mwaka 2022/23 na unatarajiwa kukamilika 2024/25 ambao unalengo la kuimarisha usafi wa mazingira katika mikoa ya Zanzibar ili kulinda afya za wenyeji na wageni. Mradi unakusudia kuanzisha mbinu madhubuti za mfumo wa udhibiti wa maji taka kuanzia Manispaa ya Mjini ikiwemo Mji Mkongwe, Michenzani, Kilimani na Kikwajuni (Mjerumani). Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali ambapo kwa mwaka 2022/23 umepangiwa kiasi cha TZS 7.8 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kujenga na kukarabati miundombinu ya maji taka;

ii. Kufanya manunuzi ya zana na vifaa;

iii. Kufanya utafiti na kusimamia maji taka;

iv. Kuajiri Mshauri Elekezi wa mradi;

v. Usimamizi na uendeshaji wa mradi; na

vi. Kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na mradi.

Mradi wa Kuimarisha Uzalishaji wa Idara Maalum za SMZ

Mradi wa Kuimarisha Uzalishaji wa Idara Maalum za SMZ umeanzishwa mwaka 2022/23 na unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili kwa gharama ya TZS 6.56 bilioni. Mradi una lengo la kuimarisha ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo zaidi kwenye Idara Maalum za SMZ ili kuleta

tija kwao na jamii kwa ujumla. Mradi unatekelezwa kwa kutumia fedha za Serikali na kwa mwaka 2022/23, umepangiwa jumla ya TZS 3.72 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Uwekaji wa miundombinu ya ufugaji kuku na ng'ombe Hanyegwa mchana na Langoni kwa Unguja na Kangagani kwa Pemba;
ii. Ununuzi wa kuku na ng'ombe wa kisasa;
iii. Ununuzi wa chakula (malisho) na dawa;
iv. Kujenga mfumo wa kuzalisha vifaranga na kuandaa shamba la kuku mama 20,000 katika kambi ya KVZ ya Muyuni;
v. Kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji katika bonde la kilimo cha mpunga Msaani - Pemba na Cheju - Unguja;
vi. Kufanya mafunzo ya ufugaji na usimamizi wa kuku na ng'ombe pamoja na kilimo cha umwagiliaji; na
vii. Kujenga kiwanda cha mikoba.

9.5.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar

Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ina jukumu la kuimarisha huduma za usajili wa matukio ya kijamii kwa kupunguza muda wa upatikanaji wa hati za usajili wa matukio ya kijamii kwa mujibu wa sheria ikiwemo mifumo ya usajili wa taarifa za vizazi, vifo, ndoa, talaka pamoja na vitambulisho vya Mzanzibar mkaazi. Kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo utakaogharimu kiasi cha TZS 1.1 bilioni zinazotarajiwa kutolewa na Serikali.

Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili

Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili umeanzishwa mwaka 2021/22 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26 na utagharimu jumla ya TZS 7.0 bilioni. Mradi una lengo la kuimarisha taarifa na usalama wa mfumo wa usajili wa taarifa za matukio ya kijamii (CRVS) na mfumo wa vitambulisho mbali mbali (Multi IDs). Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali ambapo kwa mwaka 2022/23 umepangiwa kiasi cha TZS 1.1 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuimarisha Mfumo wa 'Civil Registration and Vital Statistics' (CRVS);
ii. Kuimarisha mfumo wa vitambulisho mbali mbali (Multi IDs); na
iii. Uingizaji wa nyaraka ngumu katika mfumo wa usajili.

9.5.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ kina lengo la kuimarisha ulinzi, usalama wa raia na maliasili za bahari, kuzuia magendo ya aina zote kwa njia zinazoweza kutumika kwa kipitishia magendo, kupambana na uhalifu unaofanywa kupitia baharini ukiwemo ule wa usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya. Kwa mwaka 2022/23, Kikosi hiki kimepanga kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 14.42 bilioni kutoka Serikalini.

Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Uzamiaji na Uokozi

Mradi wa Kuimarisha Huduma za Uzamiaji na Uokozi umeanzishwa mwaka 2021/22 kwa gharama ya jumla TZS 5.3 bilioni. Mradi una lengo la kuimarisha huduma na mazingira mazuri ya kukabiliana na maafa ya baharini Unguja na Pemba yanayosababishwa na majanga ya kuzama kwa meli za abiria na mizigo na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini. Mradi unatekelezwa kupitia fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2022/23, umepangiwa jumla ya TZS 2.1 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa vituo viwili vya uzamiaji na uokozi Kizimkazi - Unguja na Wete - Pemba.

Mradi wa Uwekaji wa Rada

Mradi wa Uwekaji wa Rada umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama katika ukanda wa bahari ya Zanzibar. Mradi unatekelezwa kupitia fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2022/23, umepangiwa jumla ya TZS 9.3 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ununuzi wa rada mbili eneo la Sengenya - Pemba na Masingini - Unguja.

Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM

Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM umeanzishwa mwaka 2016/17 na unatarajiwa kutumia jumla ya TZS 12.0 bilioni mpaka kukamilika kwa mradi. Mradi una lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha wafanyakazi wa Idara Maalum za SMZ kuwa na huduma nzuri na mazingira bora ya kazi. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2022/23, umetengewa kiasi cha TZS 3.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuanza ujenzi wa mahanga katika kambi ya Bwefum;

ii. Ujenzi wa nyumba za maafisa Wete - Pemba; na

iii. Ujenzi wa ofisi za utawala – Kibweni.

9.5.3 Kikosi cha Valantia

Kikosi cha Valantia ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ kina lengo la kudhibiti hali ya usalama na amani ndani ya nchi, kukabiliana na maafa yoyote yatakayojitokeza na kuathiri jamii, kutoa huduma ya ulinzi kwa kushirikiana na vikosi vya SMZ na SMT kusaidia kutoa huduma wakati wa majanga na pia kushiriki katika shughuli za kijeshi wakati wa dharura. Kwa mwaka 2022/23, Kikosi kimepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo utakaogharimu jumla ya TZS 3.17 bilioni kutoka Serikalini.

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari umeanzishwa mwaka 2017/18 unatarajiwa kutumia jumla ya gharama TZS 5.47 bilioni. Mradi una lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa Idara Maalum za SMZ zinapata majengo mazuri ili kuimarisha utendaji wa kazi kwa wafanyakazi wake. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee ambapo kwa mwaka 2022/23, umetengewa kiasi cha TZS 3.17 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa Ofisi na nyumba ya Mkuu wa kambi ya Pujini - Pemba na Kikungwi - Unguja;

ii. Ujenzi wa hanga, nyumba na kibanda cha walinzi katika kambi ya Micheweni - Pemba;

iii. Ujenzi wa kituo cha afya na uzio katika kambi ya Ndugukitu - Pemba;
iv. Ujenzi wa kituo cha mafuta, Ofisi na hanga katika kambi ya Kiashange - Pemba; na
v. Ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za mradi.

9.5.4 Chuo cha Mafunzo

Chuo cha Mafunzo ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ chenye kutoa huduma za urekebishaji tabia kwa wanafunzi wa chuo hicho ili watakaporejea katika jamii wawe raia wema. Pia kutoa huduma salama zenye kuzingatia haki, kuongeza ubunifu katika urekebishaji kwa kubuni programu mbali mbali zitakazoweza kuwasaidia wanafunzi kujiendeleza na kujitegemea wanaporejea katika jamii. Kwa mwaka 2022/23, chuo kimepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo utakaogharimu jumla ya TZS 2.23 bilioni kutoka Serikalini.

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga umeanzishwa mwaka 2017/18 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25 ukiwa na jumla ya gharama ya TZS 8.21 bilioni kwa lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Idara Maalum za SMZ wanafanya kazi zao katika mazingira mazuri. Kwa mwaka 2022/23, mradi umetengewa kiasi cha TZS 2.23 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kumalizia ujenzi wa kambi ya Makao Makuu - Unguja; na
ii. Kuanza ujenzi wa kambi ya Bumbwini.

9.5.5 Jeshi la Kujenga Uchumi

Jeshi la Kujenga Uchumi ni miongoni mwa Idara Maalum za SMZ inayoshughulikia kutoa huduma za ulinzi kwa taasisi, kampuni na mashirika ya SMZ na SMT pamoja na yale ya binafsi au sehemu zilizo nyeti kwa usalama wa taifa, kuwafundisha vijana wa Zanzibar kulihudumia taifa lao. Aidha, kuwapatia vijana mafunzo ya msingi ya kujiendeleza katika shughuli za kilimo, viwanda, uvuvi, ufundi na kazi za amali, kuwafunza na kushiriki katika shughuli za maendeleo ya kijamii na kazi za amali, mila, utamaduni na uzalendo. Kwa mwaka 2022/23, Kikosi kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 5.46 bilioni kutoka Serikalini.

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU umeanzishwa mwaka 2017/18 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25 ukiwa na jumla ya gharama TZS 15.54 bilioni. Mradi una lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Idara Maalum za SMZ wanafanya kazi zao katika mazingira mazuri. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa kuanzia umepanga kutekeleza shughuli zake katika kambi za Pemba. Kwa mwaka 2022/23, mradi umetengewa kiasi cha TZS 3.25 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa Ofisi Kuu ya Wawi - Pemba;

ii. Kukamilisha ujenzi wa mahanga mawili na Ofisi ya Chambani - Pemba; na

iii. Kukamilisha ujenzi wa mahanga mawili na Ofisi ya Bambi Kim - Unguja.

Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa JKU

Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa JKU umeanzishwa mwaka 2022/23 unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili (2022-2023) ukiwa na jumla ya gharama TZS 3.2 bilioni. Mradi una lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Ofisi ya Wakala wa JKU wanafanya kazi zao za ulinzi kwa umahiri katika mazingira stahiki. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee ambapo kwa mwaka 2022/23, mradi umetengewa kiasi cha TZS 2.2 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuanza na ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa JKU – Mtoni.

9.5.6 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni miongoni mwa Idara maalum za SMZ ina jukumu la kusimamia shughuli zote za uzimaji moto na uokozi wa maisha na mali za wananchi, kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma za zimamoto na uokozi kwenye maeneo tofauti Unguja na Pemba zinaenda sambamba na matakwa kulingana na sheria za kitaifa na kimataifa. Kwa mwaka 2022/23, Kikosi hiki kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu kiasi cha TZS 6.0 bilioni.

Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari

Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari umeanzishwa mwaka 2017/18 na unatarajiwa kukamilika 2024/25 ukiwa na jumla ya gharama ya TZS 8.81 bilioni. Mradi ulianzishwa kwa lengo la kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Idara Maalum za SMZ wanafanya kazi zao katika mazingira mazuri. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2022/23, umetengewa kiasi cha TZS 4.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuanza ujenzi wa vituo na mahanga mawili maeneo ya Paje, Kiwengwa na Kibuteni kwa Unguja na Tasini kwa Pemba; na

ii. Kufanya ukarabati wa vituo na mahanga maeneo ya Marumbi na Kigunda kwa Unguja na Chanjaani kwa Pemba.

Mradi wa Ununuzi wa Magari na Vifaa vya Kuzimia Moto

Mradi wa ununuzi wa magari ya zimamoto na uokozi umeanzishwa mwaka 2021/22 unatarajiwa kukamilika mwaka 2022/23 ukiwa na jumla ya gharama TZS 4.0 bilioni. Mradi una lengo la kukabiliana na maafa yanayosababishwa na majanga ya moto kwa wananchi na mali zao, majanga yanayotokana na meli za abiria na mizigo na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini na nchi kavu. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2022/23, umetengewa kiasi cha TZS 2.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ununuzi wa magari mawili ya kuzimia moto.

9.6 Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais

Ofisi hii ina lengo la kuratibu na kusimamia shughuli za sekta mtambuka zikiwemo Mazingira, Ukimwi, Watu wenye mahitaji maalum na udhibiti wa madawa ya kulevya. Kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kutekeleza miradi mitatu itakayogharimu jumla ya TZS 5.61 bilioni (TZS 4.5 bilioni kutolewa na Serikali na TZS 1.11 bilioni kutolewa na Washirika wa Maendeleo).

Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuweza kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa pwani, kuyafanyia tathmini maeneo yaliyo hatarini kutokana na mabadiliko ya tabianchi, pamoja na kushajihisha uhifadhi wa mazingira kwa maendeleo endelevu ili kurejesha uoto wa kijani. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja 2022/23 na umepangiwa jumla ya TZS 4.5 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuendeleza maeneo sita yaliyoharibika kimazingira kutokana na mabadiliko ya tabianchi kwa kujenga ukuta, matuta na njia za kupunguza athari pembezoni mwa fukwe (Bwefum na Kizimkazi kwa Unguja, Sipwese, Kojani na Kisiwa Panza kwa Pemba);
ii. Kushajihisha uhifadhi wa mazingira kwa kuifanya Zanzibar ya kijani kwa kupanda miti, kuboresha uoto wa asili pamoja na uhifadhi wa vyanzo vya maji kwa kila Wilaya Zanzibar; na
iii. Kufanya tathmini kwa maeneo yalioathirika na mabadiliko ya tabianchi Zanzibar.

Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii ya Pwani

Mradi umeanzishwa mwaka 2021/22 na unatarajiwa kumalizika mwaka 2023/24 ambapo unatarajiwa kutumia jumla ya TZS 2.32 bilioni. Mradi una lengo la kuendeleza shughuli za uimarishaji wa uhimili wa mabadiliko ya tabianchi Unguja na Pemba. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund). Kwa mwaka 2022/23 mradi umepangiwa jumla ya TZS 796.03 milioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuwajengea uwezo jamii juu ya uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kupitia kilimo kinachostahamili ukame;
ii. Kujenga bwawa la kuhifadhia maji kwa ajili ya kilimo katika eneo la Bumbwini Mafufuni; na
iii. Kusaidia jamii kwa kuanzisha shughuli mbadala za kujipatia kipato kwa walengwa wa mradi ikiwemo kilimo cha mboga mboga, ufugaji wa samaki, vitalu vya miti na ufugaji wa nyuki.

Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mfumo wa Ikolojia Vijijini

Mradi huu una lengo la kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mfumo wa ikolojia vijijini ili kuepusha athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Mradi unatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja 2022/23 kwa fedha za Washirika wa Maendeleo kutoka Mfuko wa Dunia wa Mazingira (Global Environment Facility GEF) kupitia shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira (United Nations Environment Programme-UNEP). Kwa mwaka 2022/23 mradi umepangiwa jumla ya TZS 318.62 milioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuandaa mpango shirikishi wa maliasili za bahari kwa eneo la hifadhi ya ghuba - Pemba Channel Convservation Area (PECCA);
ii. Kuweka mfumo wa usimamizi wa taka zinazoathiri mazingira ya bahari; na
iii. Kusaidia jamii kwa kuanzisha shughuli mbadala zikiwemo kilimo cha mwani na kusarifu madagaa ili kujipatia kipato kwa walengwa wa mradi.

9.6.1 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya

Mamlaka ina dhamana ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulevya ikiwemo usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya, kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za dawa za kulevya na kutoa kinga, tiba na marekebisho ya tabia pamoja na mafunzo ya ujasiriamali kwa walioamua kuachana na matumizi ya dawa za kulevya. Kwa mwaka 2022/23, Mamlaka imepanga kutekeleza mradi mmoja unaotarajia kutumia jumla ya TZS 3.64 bilioni kutoka Serikalini.

Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya

Mradi huu umeanza utekelezaji wake awamu ya pili (II) mwaka 2018/19 na uantarajiwa kumalizika mwaka 2022/23. Mradi una lengo la kuimarisha kituo cha matibabu na kurekebisha tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali pekee na kwa mwaka 2022/23, umepangiwa kiasi cha TZS 3.64 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kukamilisha jengo la kituo cha tiba na marekebisho ya tabia – Kidimni;

ii. Kujenga jengo la utawala katika kituo cha tiba – Kidimni;

iii. Kujenga nyumba za wafanyakazi; na

iv. Ujenzi wa viwanja viwili vya michezo katika kituo cha tiba - Kidimni.

9.7 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi

Ofisi hii ina jukumu la kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar sambamba na kusimamia shughuli za Muungano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kufuata misingi ya katiba na sheria pamoja na kulinda haki za binadamu na ushirikishwaji. Kwa mwaka 2022/23, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja itakayogharimu jumla ya TZS 14.74 bilioni ambapo TZS 100 milioni kutoka Serikalini na TZS 14.64 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu (TASAF III) Kipindi cha Pili

Programu hii ni ya Kitaifa ambayo inatekelezwa baina ya Tanzania Bara na Zanzibar inagharimu jumla ya TZS 112.2 bilioni. Programu imeanza utekelezaji kwa awamu ya tatu mwaka 2020/21 na inatarajiwa kumalizika ifikapo mwaka 2024/25, ina lengo la kuziwezesha kaya masikini zaidi kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu ya kibinadamu hasa chakula, afya na elimu. Programu inakusudia kutekeleza miradi iliyoibuliwa na wananchi katika nyanja mbali mbali za elimu, afya, maji safi na ajira za muda kwa lengo la kuwawezesha wananchi ili waweze kujikwamua na umasikini. Kwa mwaka 2022/23, programu hii imepangiwa kiasi cha TZS 14.74 bilioni ambazo (TZS 100 milioni kutoka Serikalini na TZS 14.6 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kuratibu shughuli za TASAF baina ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara;

ii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa mradi wa TASAF; na

iii. Kuandaa mikutano ya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Wataalamu.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo

i. Kuratibu Mpango wa kuwawekea akiba na kukuza uchumi kwa walengwa wa kaya masikini;
ii. Kuanza ujenzi wa kituo cha afya Uzi kwa Unguja na Skuli ya Piki kwa Pemba; na
iii. Kufanya malipo ya fedha kwa kaya masikini (walengwa wa mradi).

9.8 Wizara ya Afya

Wizara ya Afya ina jukumu la kuhakikisha kuwa Wazanzibari wote wanapata huduma bora za afya mijini na vijijini. Sekta hii inalenga kutekeleza lengo la Dira ya Zanzibar ya 2050 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) kwa kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za afya zilizo bora na za kisasa kwa kuzingatia makundi maalum ikiwa na shabaha ya kuimarisha uwezo wa sekta ya afya na taasisi zake juu ya upatikanaji wa huduma bora za afya. Kwa mwaka 2022/23, Wizara ya Afya imepanga kutekeleza programu nne na miradi miwili yenye jumla ya TZS 60.72 bilioni ambapo Serikali imetenga jumla ya TZS 25.19 bilioni na Washirika wa Maendeleo TZS 35.53 bilioni.

Programu ya Kumaliza Maradhi ya Malaria Zanzibar

Programu ina lengo la kutokomeza maradhi ya malaria kwa kuhakikisha kwamba maradhi haya yanamalizika kabisa katika visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha, programu inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2022/23 programu imepangiwa jumla ya TZS 3.93 bilioni (TZS 513 milioni kutoka Serikalini na TZS 3.42 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Ununuzi wa dawa za kutibu ugonjwa wa malaria;
ii. Ununuzi wa viuatilifu vya viluilui;
iii. Ununuzi wa ndege nyuki (drone);
iv. Ununuzi wa vitendanishi vya uchunguzi wa vimelea vya malaria; na
v. Uchukuaji wa hatua ya haraka kwa maeneo yanayotoka wagonjwa wa malaria.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Utibabu na uchunguzi wa maradhi ya malaria;
ii. Udhibiti wa mbu waenezao malaria;
iii. Ufuatiliaji na tathmini ya ugonjwa wa malaria; na
iv. Uhamasishaji jamii juu ya kujikinga na maradhi ya malaria.

Programu Shirikishi ya Huduma za Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto

Programu ina lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Programu inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo ambapo jumla ya TZS 3.23 bilioni zitatumika (TZS 1.52 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.71 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa mwaka 2022/23.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kuimarisha huduma za mama na watoto chini ya miaka mitano na watoto wachanga;
ii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi na kupunguza vifo vya mama na mtoto;
iii. Kuimarisha upatikanaji wa taarifa za mama na mtoto; na
iv. Kuimarisha huduma za damu salama.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo

i. Kuimarisha huduma za mama na watoto chini ya umri wa miaka mitano na watoto wachanga;
ii. Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo na vifo vya mama na mtoto; na
iii. Kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo za mama na mtoto.

Programu ya Kudhibiti Maradhi ya UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma

Programu hii inajumuisha miradi ya kupambana na maambukizi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua kikuu na Ukoma. Lengo la programu ni kupunguza na kudhibiti kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI, kupunguza vifo

vinavyotokana na maradhi ya kifua kikuu na kupunguza maambukizi ya ukoma. Programu inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo ambapo jumla ya TZS 5.03 bilioni (TZS 94.28 milioni kutoka Serikalini na TZS 4.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepangwa kutumika kwa mwaka 2022/23.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma; na

ii. Kuimarisha huduma za UKIMWI kwa makundi maalum na makundi hatarishi.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za kinga na tiba ya homa ya ini;

ii. Kuimarisha huduma za matibabu kwa watu na makundi maalumu wanaoishi na VVU;

iii. Kuimarisha ugunduzi wa wagonjwa wa ukoma na kuwapa matibabu sahihi;

iv. Kuimarisha utoaji wa huduma za matibabu kwa wagonjwa wanoishi na virusi vya UKIMWI;

v. Kuimarisha huduma ya utoaji wa kinga ya maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto; na

vi. Kuimarisha matumizi ya takwimu bora za HIV, homa ya ini, kifua kikuu na ukoma.

Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya

Programu ina lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba kwa hospitali za Wilaya na Mikoa kwa ajili ya kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za afya kwa wananchi Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa kutekeleza jumla ya miradi sita kwa gharama za TZS 36.67 bilioni.

Mradi wa Kuzipandisha Hadhi Hospitali za Wilaya na Hospital za Vijiji

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba kwa hospitali za Wilaya na Mikoa kwa ajili ya

kuimarisha ubora wa utoaji wa huduma za afya kwa wananchi Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2022/23, mradi umetengewa kutumia jumla ya TZS 8.95 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa chumba cha wagonjwa mahututi katika hospitali ya Abdalla Mzee - Pemba;
ii. Kumalizia ujenzi wa wodi ya mama na mtoto hospitali ya Chake Chake - Pemba;
iii. Ununuzi wa vifaa tiba katika hospitali ya Chake Chake - Pemba; na
iv. Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi hospitali ya Abdalla Mzee - Pemba;

Mradi wa Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa - Unguja

Mradi huu umeanza mwaka 2021/22 ukiwa na lengo la kujenga bohari kubwa na ya kisasa ya kuhifadhia dawa na vifaa tiba Unguja katika eneo la Maruhubi. Mradi huu umekadiriwa kutumia jumla ya TZS 5.4 bilioni kutoka Serikalini ambapo kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 3.5 bilioni zimetengwa.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa bohari ya kuhifadhia dawa na vifaa tiba - Maruhubi.

Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa - Unguja

Mradi umeanza mwaka 2020/21 ukiwa na lengo la kuimarisha uchunguzi, ubora na usalama wa bidhaa za dawa na vipodozi ili kuepuka kusambaa kwa dawa zisizo na ubora na bandia katika soko la Zanzibar. Kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 4.46 bilioni zimetengwa kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ununuzi wa vifaa vya maabara na samani (ZFDA).

Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya 'Biochemistry'

Mradi umeanzishwa mwaka 2021/22 na unatekelezwa katika Taasisi ya Utafiti wa Afya kwa lengo la kuimarisha Taasisi hiyo kuweza kufanya tafiti mbali mbali ili kupata taarifa zitakazoisaidia sekta ya afya kufanya maamuzi sahihi katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya katika nchi yetu. Mradi umekadiriwa kutumia TZS 6.0 bilioni kutoka Serikalini hadi kukamilika

kwake na kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 4.50 bilioni zimepangwa kutumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa jengo la maabara ya Bio-chemistry – Binguni.

Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wete

Mradi una lengo la kuwa na hospitali ya kisasa ambayo itahudumia wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na maeneo ya jirani. Mradi unatekelezwa na Serikali kwa mashirikiano na Washirika wa Maendeleo na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 23.00 bilioni. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.74 bilioni (TZS 100 milioni kutoka Serikalini na TZS 3.64 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Uendeshaji na uratibu wa shughuli za mradi.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo

i. Kufanya ukarabati kwa baadhi ya majengo ya hospitali ya Wete; na
ii. Kuanza ujenzi majengo mapya ya hospitali ya Wete.

Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Mahonda

Mradi una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja na maeneo ya jirani. Mradi utaanza mwaka 2022/23 na unakadiriwa kutumia TZS 11.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa hospitali ya Mkoa katika eneo la Mahonda.

Mradi wa Bima ya Afya Zanzibar

Mradi huu una lengo la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wa Zanzibar ili waweze kupata huduma za afya kwa unafuu zaidi. Mradi umeanzishwa mwaka 2022/23 na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 9.10 bilioni mpaka kukamilika kwake. Kwa mwaka 2022/23, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 1.54 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuuwezesha Mfuko wa Bima; na
ii. Usajili wa wanachama na uchapishaji wa kadi za bima ya afya.

Mradi wa Kuwekeza katika Huduma za Mama na Mtoto

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya ya mama na mtoto. Mradi umeanza mwaka 2022/23, na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 46.0 bilioni hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka 2022/23, umepangiwa jumla ya TZS 10.3 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa

i. Uratibu na utekelezaji wa mpango wa kuimarisha huduma za mama na mtoto;
ii. Ufuatiliaji na usimamizi wa mpango wa kuimarisha huduma za mama na mtoto;
iii. Kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za mama na mtoto;
iv. Kuimarisha nguvu kazi ya afya;
v. Ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa mama na mtoto;
vi. Kuimarisha mfumo wa rufaa kwa mama wajawazito; na
vii. Kuimarisha huduma za kidigitali katika kutoa huduma za mama na mtoto.

Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazimmoja

Mradi una lengo la kuimarisha huduma zinazotolewa katika hospitali ya Mnazimmoja kwa kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa ili kutoa huduma za rufaa kwa ufanisi na zenye ubora. Mradi umeanza mwaka 2022/23, ambapo umekadiriwa kutumia jumla ya TZS 99.51 bilioni (TZS 90.90 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na TZS 8.60 bilioni kutoka Serikalini) hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 13.52 bilioni (TZS 5.55 bilioni kutoka Serikalini na TZS 7.97 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kufanya ukarabati wa hospitali ya Mnazimmoja katika jengo la wodi za wagojwa na jengo la Mapinduzi Kongwe;

ii. Ununuzi wa vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu;

iii. Ununuzi wa mitambo miwili ya kuchomea taka na mtambo wa kuzalisha oksijeni;

iv. Kununua vitendea kazi vya hospitali;

v. Kutoa mafunzo ya utumiaji wa mashine na vifaa vya uchunguzi kwa madaktari matabibu na wafanyakazi husika wa hospitali; na

vi. Uwekaji wa mfumo wa kumbukumbu za wagonjwa (eHMS).

Shughuli Zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo

i. Malipo ya awali ya Mshauri Elekezi;

ii. Malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa mradi;

iii. Kulipia gharama za uendeshaji wa shughuli za mradi; na

iv. Kufanya ukarabati wa majengo ya hospitali ya Mnazimmoja.

9.9 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi inasimamia sekta ya ardhi na makaazi ambazo zina jukumu la kuhakikisha usimamizi mzuri wa upatikanaji na matumizi ya ardhi pamoja na kuimarisha makaazi ya wananchi kwa ujenzi wa nyumba bora za kuishi zenye viwango vinavyokubalika. Aidha, Wizara inashughulika na kazi ya kuzifanyia matengenezo nyumba za maendeleo. Kwa mwaka 2022/23, Wizara hii imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu kiasi cha TZS 17.0 bilioni.

Mradi wa Matengenezo ya Nyumba za Maendeleo

Mradi huu una lengo la kuwapatia wananchi makaazi bora mijini na vijijini na utahusisha marekebisho ya miundombinu mbali mbali katika nyumba za maendeleo ikiwemo miundombinu ya maji safi na maji taka, miundombinu ya umeme, uwekaji wa madirisha na milango sambamba na ujenzi wa maegesho ya magari katika maeneo tofuati ya nyumba hizo. Kwa mwaka 2022/23, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 16.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuweka miundombinu ya umeme ikiwemo kubadilisha nyaya za ‘fitting’ ya umeme kwenye fleti sambamba na ufungaji wa taa za umeme;

ii. Kuifanyia marekebisho mifumo ya maji safi;
iii. Kufanya marekebisho ya miundombinu ya maji taka;
iv. Kufanya ukarabati kwa majengo yaliyochakaa; na
v. Kujenga maegesho ya magari kwa baadhi ya majumba.

Mradi wa Utayarishaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi

Mradi una lengo la kuwezesha wamiliki na watumiaji wa ardhi kuzingatia matumizi bora ya ardhi na uzalishaji wenye tija kwenye ardhi wanayomiliki. Mradi huu unatarajiwa kuanza utekelezaji wake mwaka 2022/23 na kukamilika mwaka 2023/24. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuandaa mpango maalum wa matumizi ya ardhi;
ii. Kufanya utambuzi wa wamiliki wa ardhi kwa ngazi ya Shehia, Wilaya na Mkoa;
iii. Kufuatilia na kutathmini mpango wa matumizi ya ardhi;
iv. Kutayarisha ramani na mabango na kusambaza katika maeneo yatakayopendekezwa; na
v. Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi katika utekelezaji wa mpango wa matumzi ya ardhi.

9.10 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Malengo makubwa ya Wizara ya Biashara na Viwanda ni kukuza viwanda vidogo na vya kati sambamba na kuimarisha mazingira bora ya ufanyaji biashara kwa lengo la kuleta maendeleo nchini. Kwa mwaka 2022/23, Wizara hii itatekeleza shughuli za maendeleo kupitia programu moja na mradi mmoja wa maendeleo kwa gharama ya TZS 15.6 bilioni. Kati ya fedha hizo, Serikali imepanga kutoa TZS 11.0 bilioni na Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia TZS 4.6 bilioni.

Programu ya Kuendeleza Viwanda

Wakala wa kusimamia na kuendeleza viwanda vidogo vidogo na vya kati (SMIDA) miongoni mwa jukumu lake ni kuwalea wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kuwapatia mafunzo ya kitaalamu katika bidhaa zao. Programu hii ilianza mwaka 2017/18 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025. Kwa

mwaka 2022/23, Programu imepangiwa jumla ya TZS 11.6 bilioni kwa ajili ya kutekeleza miradi miwili ifuatayo:-

Mradi wa Kuimarisha Maeneo Tengefu ya Viwanda (Industrial Park)

Mradi huu ulianzishwa mwaka 2020 ukiwa na lengo la kuanzisha maeneo tengefu ya viwanda ili kurahisisha viwanda vidogo na vya kati kuwepo kwenye maeneo hayo maalum yatakayosaidia kukuza uchumi na kutoa ajira kwa wajasiriamali. Kwa mwaka 2022/23, mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS 2.50 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ulipaji wa fidia kwa wenye mashamba na makaazi yatakayoathirika katika maeneo ya viwanda ikiwemo Nungwi na Dunga;
ii. Kuandaa eneo kwa ajili ya ujenzi;
iii. Kuandaa tathmini ya mradi kwa maeneo ya viwanda;
iv. Kuweka miundombinu ya maji na barabara kwenye maeneo ya viwanda; na
v. Ada ya Mshauri Elekezi na msimamizi wa ujenzi.

Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa

Lengo la mradi ni kuwasaidia wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kuwapatia mafunzo ya vitendo kwa lengo la kuwaendeleza na kuwapatia mikopo. Mradi huu ulianza mwaka 2018/19 na unatarajia kukamilika mwaka 2024/25. Mradi unatekelezwa kwa mashiriano baina ya Serikali na Mfuko wa Maendeleo kutoka falme za Kiarabu. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa jumla ya TZS 9.1 bilioni (TZS 4.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.6 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kutoa mafunzo na mikopo kwa wajasiriamali;
ii. Kuimarisha maabara ya utengenezaji thamani ya bidhaa; na
iii. Ujenzi wa kituo cha usarifu wa mazao ya kilimo.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo kwa kuwapatia mikopo nafuu;

ii. Kuwajengea uwezo wajasiriamali kwa kuwapa mafunzo ya kusarifu bidhaa zao Unguja na Pemba; na

iii. Kuwawezesha wajasiriamali kwa kuwapatia vifaa vitakavyowasaidia kuendeleza viwanda vyao.

Mradi wa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar

Mradi huu ulianza mwaka 2017/18 na unatarajia kukamilika mwaka 2024/25. Lengo la mradi huu ni kutoa huduma za kuimarisha sekta ya biashara na viwanda kwa kutoa msaada kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa jumla ya TZS 4.0 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Malipo kwa mshauri elekezi wa ujenzi uwanja wa maonyesho;

ii. Kuanza ujenzi wa uwanja wa maonyesho wa kimataifa wa Zanzibar; na

iii. Kufikisha miundombinu ya maji, umeme na TEHAMA katika eneo la mradi.

9.11 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Sekta ya Elimu ina wajibu wa kutoa elimu bora na jumuishi kwa Wazanzibari wote kwa kuwa na miundombinu wezeshi, kuongeza idadi ya walimu wenye sifa na vitabu vya kisasa vinavyoendana na maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia. Lengo ni kuimarisha rasilimali watu wenye uwezo wa kujiajiri na kuajirika ili kukidhi mahitaji ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050 na Mpango wa Maendeleeo wa Zanzibar wa 2021-2026. Kwa mwaka 2022/23, Sekta ya elimu imepanga kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo yenye jumla ya TZS 97.72 bilioni ambapo Serikali imepanga kutoa TZS 36.97 bilioni na Washirika wa Maendeleo TZS 60.74 bilioni (TZS 45.08 bilioni ni mkopo na TZS 15.66 ni ruzuku).

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha watoto wote waliofikia umri wa kuanza skuli kwa ngazi ya maandalizi na msingi wana mazingira mazuri ya kupata elimu bora. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha

za Serikali na Washirika wa Maendeleo ambapo kwa mwaka 2022/23, umepangiwa jumla ya TZS 20.96 bilioni (TZS 10.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 10.46 bilioni za Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kujenga skuli nne (mbili za msingi na mbili za maandalizi) katika Mkoa wa Mjini Magharibi na Kaskazini - Unguja, Kusini na Kaskazini - Pemba;
ii. Kukamilisha madarasa 50 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi; na
iii. Kujenga karakana za elimu amali katika skuli za elimu mjumuisho Jendele kwa Unguja na Pujini Pemba.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Washirika wa Maendeleo

i. Kuimarisha uwezo wa wanafunzi wa msingi katika kusoma, kuandika na kuhesabu;
ii. Uimarishaji wa programu ya lishe skuli za msingi 42 zilizo katika mazingira magumu Unguja na Pemba;
iii. Kukamilisha mihutasari ya elimu ya maandalizi na msingi;
iv. Ununuzi wa vitabu pamoja na kuwapatia mafunzo walimu wote wa maandalizi na msingi kufuatia kukamilika kwa mitaala mipya ya elimu ya maandalizi na msingi; na
v. Kuzipatia vifaa vya elimu ya ufundi skuli za elimu mjumuisho za Jendele na Pujini.

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima

Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kila mtoto anapatiwa haki yake ya elimu katika ngazi ya sekondari ya lazima. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo ambapo kwa mwaka 2022/23, umepangiwa jumla ya TZS 43.52 bilioni (TZS 21.98 bilioni kutoka Serikalini na TZS 21.54 bilioni za Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kuimarisha mifumo ya teknolojia katika skuli, vituo vya walimu na vituo vya ubunifu;
ii. Kuimarisha miundombinu ya vyuo vya ualimu vya Mazizini Unguja na Kiuyu Pemba pamoja na kuvipatia vifaa;

iii. Kujenga uzio katika skuli ya sekondari ya Kibuteni Unguja na Mohammed Juma Pindua kwa upande wa Pemba;

iv. Kujenga skuli moja ya sekondari ya ufundi pamoja na kuipatia vifaa;

v. Kufanya ukarabati mkubwa wa skuli za sekondari za ufundi Mikunguni - Unguja na Kengeja - Pemba;

vi. Kuimarisha huduma za maktaba kwa kujenga maktaba ya Wilaya ya Kaskazini B katika eneo la Kinduni; na

vii. Kujenga Ofisi ya ukaguzi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja pamoja na kuzipatia usafiri Ofisi mbili za ukaguzi za kanda.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Kuzipatia skuli vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vya wanafunzi wenye mahitaji maalum;

ii. Kutoa mafunzo kwa walimu wa sekondari kwa masomo ya Sayansi, Hisabati na Kiingereza;

iii. Kuwajengea uelewa walimu na wanafunzi juu ya elimu ya afya ya uzazi na stadi za maisha;

iv. Kuzipatia skuli ruzuku ya fedha kwa ajili ya gharama za uendeshaji;

v. Kuandaa Mpango Mkuu wa Elimu wa miaka mitano (2022 - 2027);

vi. Kujenga skuli tatu za sekondari zenye dakhalia kwa mashirikiano na BADEA katika maeneo ya Gamba, Mfenesini na Kifundi;

vii. Kujenga skuli tatu za sekondari katika maeneo ya Bumbwini, Kisiwandui kwa Unguja na Shamiani kwa Pemba;

viii. Kujenga maabara katika skuli 10 za sekondari Unguja na Pemba; na

ix. Kujenga dakhalia katika skuli tatu za Paje Mtule na Lumumba kwa Unguja na Chwaka Tumbe kwa Pemba;

Mradi wa Kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali

Lengo la mradi ni kutoa elimu ya amali ili kupunguza utegemezi wa ajira Serikalini na kuwa na wataalamu wazalendo katika fani mbali mbali. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha za Serikali na Washirika wa Maendeleo ambapo kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 33.25 bilioni (TZS 4.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 28.75 bilioni za Washirika wa Maendeleo) zimetengwa.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kuvipatia vyuo vya Amali vifaa vya kisasa ili viweze kutoa mafunzo ya vitendo na nadharia; na
ii. Kufanya ukarabati wa Chuo cha Elimu Mbadala Rahaleo.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Kujenga vyuo vitano vya mafunzo ya amali katika maeneo ya Fumba, Jendele, Mangapwani, Tumbe na Chambani; na
ii. Kujenga Chuo cha ubaharia katika eneo la SUZA Kampasi ya Nkurumah.

9.12 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Lengo kuu la Wizara ni kusimamia sekta ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ili kuweza kuimarisha na kuendeleza maeneo hayo na kutatua changamoto zilizopo. Pia, Wizara ina jukumu la kuhakikisha habari zinatolewa na kupokelewa kwa usahihi na kwa wakati, kuwawezesha vijana na kuwatafutia fursa mbali mbali za ajira, kudumisha utamaduni na kuimarisha michezo kwa lengo la kuimarisha afya za wananchi na kuongeza ajira. Kwa mwaka wa 2022/23, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inatarajia kutekeleza programu tatu na miradi miwili yenye jumla ya TZS 32.73 bilioni kutoka Serikalini.

Programu ya Ajira kwa Vijana

Programu hii ina lengo la kuweka mazingira mazuri na endelevu kwa vijana ili waweze kujiimarisha kiuchumi na kijamii kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali ya kitaalamu pia waweze kuwa wabunifu na kujiari wenyewe sambamba na kujipatia kipato chenye tija kwa kujiendesha na maisha yao ya kila siku. Programu hii imeanza mwaka 2021/22 na inatarajia kumaliza 2024/2025. Kwa mwaka 2022/23, Programu imepangiwa jumla ya TZS 6.4 bilioni Fedha kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa vituo viwili vya maendeleo ya vijana katika enel la Muyuni - Unguja na Pujini - Pemba.

Programu ya Uimarishaji wa Utoaji wa Matangazo (ZBC)

Lengo la programu ni kuimarisha mfumo wa matangazo ili kuweza kusikika kwa urahisi ndani na nje ya nchi. Programu imeanza mwaka 2021 na inatarajia kuisha mwaka 2025, Kwa mwaka 2022/23, Programu inatarajia kutumia jumla ya TZS 12.32 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa jengo jipya la Shirika la Utangazaji Tunguu Zanzibar;
ii. Ujenzi wa uzio na uwekaji wa lifti Mkanjuni Pemba;
iii. Ununuzi wa majenereta mawili ya Ofisi kwa Unguja;na
iv. Ununuzi wa gari sita za Shirika.

Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo

Dhumuni la programu ni kukuza na kuendeleza Michezo Zanzibar na kuifanya sekta ya michezo kuweza kuimarika zaidi. Programu imeanza 2021/2022 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025-2026. Kwa mwaka 2022/23 programu hii imepangiwa jumla ya TZS 7.0 bilioni kwa ajili ya kutekeleza miradi mikuu miwili.

Mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo

Lengo la mradi huu ni kuiwezesha sekta ya michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar itakayokidhi viwango vya kimataifa. Mradi huu umeanza 2021 hadi 2025, kwa mwaka wa fedha 2022/23 mradi unatarajiwa kutumia jumla ya TZS 4.0 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa vyumba vya wachezaji katika uwanja wa Mao Zedong na kuongeza ukuta;
ii. Kufanya ukarabati wa uwanja wa Gombani; na
iii. Uwekaji wa uzio katika viwanja vya Wilaya Kitogani-Unguja, Kishindeni na Kangani kwa Pemba.

Mradi wa Ujenzi wa Viwanja na Vyuo vya Michezo

Lengo la mradi ni kuibua na kuendeleza vipaji vya wanamichezo hususan vijana kwa kuweka miundombinu yenye kuhusisha aina mbali mbali za michezo ili kuongeza ushindani wa kimichezo kitaifa na kimataifa. Kwa mwaka 2022/23, mradi huu umepangiwa TZS 3.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa bwawa la kuogelea katika uwanja wa Amani;

ii. Ujenzi wa viwanja viwili vya michezo midogo midogo (4 in 1) kwa Pemba Wilaya ya Micheweni skuli ya Micheweni na Wilaya ya Chake –Chake Gombani; na

iii. Ujenzi wa akademia ya michezo katika kijiji cha Mwehe- Makunduchi.

Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa

Lengo kuu la mradi ni kuweka miundombinu imara ya sanaa mbali mbali na kuwapatia mafunzo wasanii wa Zanzibar ili waweze kutoa kazi zenye ubora na kuweza kujiajiri. Mradi umeanza 2022/23 hadi 2025/26 na unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2022/23, umepangiwa kiasi cha TZS 5.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa nyumba ya sanaa katika eneo la Mwanakwerekwe; na

ii. Ununuzi wa samani na vifaa vya Ofisi za nyumba ya sanaa.

Mradi wa Uendelezaji wa Mitambo ya Kisasa ya Uchapaji

Dhumuni la mradi ni kuimarisha Wakala wa Serikali wa Uchapishaji ili aweze kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa machapisho na kuboresha bohari kuu ya Serikali. Mradi umeanza mwaka 2021/25 na kwa mwaka 2022/23 mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ununuzi wa mitambo na vifaa vya uchapaji; na

ii. Kuwajengea uwezo mafundi wa mitambo kwa kuwapatia mafunzo ili kuongeza ufanisi katika kazi.

9.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

Wizara hii inahusisha sekta kuu nne ambazo zinasaidia katika kujikimu kimaisha pamoja na kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora. Sekta hizo ni miongoni mwa sekta muhimu katika ukuzaji wa uchumi kwa kutoa mchango wa moja kwa moja kwa wananchi katika kupambana na umasikini kwa kuwapatia chakula, ajira pamoja na kuimarisha huduma za kilimo. Aidha Wizara ina jukumu la kusaidia upatikanaji wa mbegu na utoaji wa mafunzo

kwa wakulima na wafugaji. Kwa mwaka 2022/23, Wizara imepanga kutekeleza programu tatu za maendeleo zenye jumla ya TZS 30.34 bilioni kati ya fedha hizo (TZS 8.69 bilioni ni kutoka Serikalini na TZS 21.25 bilioni mkopo na TZS 388 milioni ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Programu ya Umwagiliaji

Programu ya Umwagiliaji awamu ya pili imeanzishwa kwa lengo la kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji. Program hii itaanza utekelezaji wake mwaka 2022/23 na inatarajiwa kukamilika 2023/24 ambapo itagharimu jumla ya TZS 40.0 bilioni. Kwa mwaka 2022/23 inatarajiwa kutumia jumla ya TZS 20.50 bilioni (TZS 500 milioni kutoka Serikalini na TZS 20.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kufanya malipo ya fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;
ii. Kuunga umeme wa njia kuu (3-phase) kwa visima 15 katika bonde la Cheju B; na
iii. Kumalizia kazi ya kuunga umeme katika bonde la Kibokwa na Kilombero.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Kuendelea na ujenzi na usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa hekta 370 katika bonde la Cheju “B”; na
ii. Kuendelea na ujengaji wa misingi ya ndani (Tertiary canals) kwa kiwango cha saruji katika bonde la Cheju A, Kinyasini, Kilombero, Kibokwa, Chaani kwa Unguja na Mlemele kwa Pemba.

Programu ya Kudhibiti Maradhi na Upotevu wa Mazao

Programu imeanzishwa kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo ili kuongeza upatikanaji wa chakula kwa wakulima na wananchi nchini. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa jumla ya TZS 3.84 bilioni (TZS 2.19 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.64 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa kutekeleza miradi miwili.

Mradi wa Kudhibiti Sumu Kuvu Inayotokana na Ulaji wa Mahindi na Njugu

Mradi una lengo la kupuguza athari zinazotokana na sumukuvu katika mahindi na njugu nyasa kwa kutoa taaluma na kuimarisha miundombinu na teknologia kabla na baada ya mavuno. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara na unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2019 - 2024). Kwa mwaka 2022/23, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 1.25 bilioni ikiwa ni mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kukamilisha ujenzi wa maghala mawili na uwekaji wa vifaa vya kuhifadhia mazao ya nafaka katika eneo la Kizimbani - Unguja na Ole Dodeani - Pemba;
ii. Kutoa mafunzo ya udhibiti wa sumukuvu kwa wadau wa mnyororo wa thamani wa mazao ya mahindi na njugu nyasa; na
iii. Kuendelea kuwapa mafunzo ya utengenezaji wa vizimba vya chuma vijana 40 kwa Unguja na Pemba, mafunzo hayo ni kwa mashirikiano baina ya VETA na Mamlaka ya Ufundi Stadi Zanzibar (VTA) pamoja na utoaji wa teknolojia ya darasa za kukaushia.

Mradi wa Kudhibiti Upotevu wa Mazao

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo ili kuongeza kasi ya upatikanaji wa chakula kwa wakulima na wananchi wa Zanzibar. Mradi unajumuisha uwezeshaji kwa wakulima ili kupata masoko baada ya mavuno kwa kuongeza thamani na kipato kwa mazao ya kilimo. Mradi unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka minne 2022-2026 na utagharimu jumla ya TZS 10.07 bilioni ambapo kwa mwaka 2022/23 umepangiwa jumla ya TZS 2.58 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Kuanzisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za upotevu wa mazao ya kilimo;
ii. Kuwezesha mfumo wa masoko ya kilimo ili kuboresha upatikanaji wa masoko kwa bidhaa zinazozalishwa nchini;
iii. Kuwawezesha wakulima kwa kuwapatia vifaa vya kuchakata mazao ya kilimo kwa Wilaya za Unguja na Pemba; na
iv. Kununua vifaa vya kukusanyia sampuli za wadudu wa matunda.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Kutengeneza mitego ya kunasia nzi wa matunda katika Maabara ya wadudu iliyopo Kizimbani; na
ii. Kununua vifaa vya kuimarisha mfumo wa uingizaji na utoaji wa mazao, vifaa vya maabara ya karantini na dawa za kunasia nzi wa matunda.

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo

Programu ina lengo la kuimarisha na kuinua sekta ya kilimo na mifugo kwa wafugaji wadogo wadogo nchini. Kwa mwaka 2022/23 programu hii itajumuisha miradi miwili itakayagharimu jumla ya TZS 6.0 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza miradi ifuatayo:

Mradi wa Kurejesha Urithi wa Kijani

Mradi una lengo la kuendeleza urithi wa kijani wa Zanzibar kwa uzalishaji wa miche ya miti ya misitu na matunda sambamba na upandaji wa miti katika maeneo ya wazi ya mashamba ya Serikali, maeneo yaliyoathirika na uchimbwaji wa maliasili zisizorejesheka na maeneo ya misitu ya jamii kurejea katika haiba yake. Mradi unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili (2022-2024) na utagharimu jumla ya TZS 2.65 bilioni. Kwa mwaka 2022/23, mradi huu umepangiwa kiasi cha TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuotesha miche bora 140,000 na kuiatika katika maeneo yaliyoathiriwa na uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka na maeneo ya misitu ya jamii;
ii. Kutayarisha maeneo na kupanda miti katika hekta 55 Unguja na Pemba; na
iii. Kuimarisha miundombinu katika vitalu vya Serikali vya uzalishaji wa miche Unguja na Pemba.

Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo

Lengo la mradi ni kuimarisha miundombinu ya mifugo ili kuongeza kasi ya uzalishaji na usalama wa mifugo inapoingia nchini pamoja na mazingira bora ya uchinjaji wa mifugo. Mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha TZS 11.2 bilioni kwa kipindi cha miaka mitatu (2021-2024) ambapo kwa mwaka 2022/23 umepangiwa jumla ya TZS 5.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa miundombinu ya karantini ya mifugo katika maeneo ya Kisakasaka na Donge kwa Unguja na Gando kwa Pemba;
ii. Ununuzi wa mtambo wa kuzalisha gesi ya naitrojeni kwa ajili ya kuhifadhia mbegu za kupandisha ng'ombe kwa sindano;
iii. Ujenzi wa chinjio la kisasa eneo la Kisakasaka Unguja;
iv. Ujenzi wa maabara ya Utafiti wa mifigo eneo la Kizimbani - Unguja na ukarabati Chamanangwe Pemba; na
v. Ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza chakula cha mifugo Kizimbani –Unguja.

9.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto imeundwa kwa lengo la kushughulikia maendeleo ya kijamii na kuleta usawa wa kijinsia sambamba na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za jamii, wazee na watoto ili kuwa na hali bora za maisha. Kwa mwaka 2022/23, sekta imepanga kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo kwa fedha za Serikali.

Mradi wa Hifadhi ya Wazee

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mazingira ya wazee wanaoishi katika makao ya wazee Unguja na Pemba kwa kuimarisha makaazi yao, usalama na upatikanaji wa huduma zao za msingi kikamilifu. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 3.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kujenga uzio kwenye makaazi ya wazee Welezo;
ii. Ukarabati wa nyumba za wazee Sebleni;
iii. Ununuzi wa vifaa na samani;
iv. Kufanya ukarabati mkubwa katika makaazi ya wazee Welezo; na
v. Kutoa elimu kwa wadau tofauti juu ya umuhimu wa kuwatunza wazee.

9.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini

Wizara ya Maji, Nishati na Madini inajumuisha sekta kuu tatu ambazo ni maji, nishati na madini. Wizara hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote zilizo chini ya sekta hizo ili kuweza kuhakikisha wakaazi wa Zanzibar wanafaidika na huduma za maji safi na salama, upatikanaji na usambazaji

wa nishati endelevu kwa ufanisi na unafuu. Kwa mwaka 2022/23, Wizara imepanga kutekeleza jumla ya programu mbili zitazogharimu kiasi cha TZS 128.70 bilioni. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 37.47 bilioni kutoka Serikalini na TZS 91.23 bilioni ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (TZS 1.70 bilioni ni ruzuku na TZS 89.53 bilioni ni mkopo).

Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar

Programu hii ina lengo la kusimamia na kuhakikisha huduma za usambazaji maji safi na salama zinapatikana katika maeneo yote ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi wote kunufaika na huduma hiyo muhimu katika jamii. Kwa mwaka 2022/23, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 106.68 bilioni (TZS 22.74 bilioni kutoka Serikalini na TZS 79.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kutekeleza shughuli zake kupitia miradi minne kama ifuatavyo:-

Mradi wa Kuendeleza Visima vya Ras el Khaimah

Mradi wa Kuendeleza Visima vya Ras el Khaimah ulianza mwaka 2016/17 ikiwa ni muendelezo wa mradi wa awali wa uchimbaji wa visima uliotekelezwa kwa mashirikiano baina ya Ras el Khaimah na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo kupitia mradi huu jumla ya visima 150 (113 Unguja na 37 Pemba) vilichimbwa. Lengo la mradi huu ni kuongeza uzalishaji wa maji katika maeneo husika ili kutosheleza mahitaji kwa wananchi. Kwa sasa mradi huu unatekelezwa na Serikali pekee ambapo kazi zinazoendelea ni uwekaji wa miundombinu ya maji ili kuhakikisha wananchi wa maeneo yaliyochimbwa visima hivyo wanapata maji safi na salama. Kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 18.15 bilioni zimepangwa kutumika.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ulipaji wa fidia kwa waathirika wa mradi;
ii. Uchimbaji na ufukiaji wa misingi;
iii. Ununuzi na ulazaji wa mabomba katika visima;
iv. Ununuzi na uwekaji wa pampu za visima;
v. Ujenzi wa matangi na vibanda vya kuendeshea pampu na wellhead;
vi. Uvutaji wa umeme kwa maeneo ya visima;
vii. Ununuzi wa compressor kwa ajili ya usafishaji wa visima; na
viii. Ununuzi wa mita za uzalishaji maji.

Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA)

Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) unalenga kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa maji safi na salama katika maeneo ya Zanzibar kupitia zoni ya Mfenesini, Kizimbani, Tunguu na Fumba. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kuwa tatizo la maji katika maeneo yaliyokusudiwa linaondoka kabisa na wananchi wanaweza kupata maji safi na salama muda wote kwa kuimarisha na kujenga miundombinu imara katika vyanzo vya maji. Mradi huu unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya India. Kwa mwaka 2022/23 mradi umepangiwa jumla ya TZS 70.36 bilioni (TZS 3.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 66.86 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Ulipaji wa fidia katika maeneo yatakayoathirika na mradi;
ii. Kufanya tathmini ya kimazingira (EIA/SEIA); na
iii. Kuratibu vikao vya Kamati Kiongozi na Kamati ya Wataalamu.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Kuendelea na kazi za uchimbaji wa visima;
ii. Kuendelea na kazi ya ujenzi wa matangi na ulazaji wa mabomba;
iii. Kuendelea na kazi ya ufungaji wa mita; na
iv. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi.

Mradi wa Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar

Mradi umeanzishwa kwa lengo kuu la kuimarisha huduma za maji safi, kuijengea uwezo ZAWA na kuongeza mapato ya Mamlaka. Aidha, mradi unalenga kuimarisha miundombinu ya maji safi na maji taka kwa lengo la kuimarisha afya za watu kwa kutoa maji safi na salama na kuyatibu maji machafu yasiweze kutoa madhara katika jamii na mazingira pamoja na kuepuka maji machafu kuingia baharini na kuharibu mazingira ya baharini. Utekelezaji wa shughuli za mradi huu utadhaminiwa na Washirika wa Maendeleo kwa gharama ya TZS 80.5 bilioni ambapo kwa upande wa Serikali utatakiwa kugharamia malipo ya fidia kwa maeneo yatakayoathirika

na mradi pamoja na kazi za uratibu wa shughuli za mradi ikiwemo ufuatiliaji na tathmini. Kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 12.48 bilioni (1.09 bilioni kutoka Serikalini na 11.39 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepangwa kutumika.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Ulipaji wa fidia kwa maeneo yatakayoathirika na mradi; na
ii. Uendeshaji wa shughuli za mradi.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Malipo ya Mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi.

Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Maji Zanzibar

Mradi wa Uimarishaji wa Huduma za Maji Zanzibar una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa kufanya upembuzi yakinifu wa kuweza kugundua kiwango cha rasilimali maji kilichoko chini ya ardhi ili kurahisisha na kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi mijini na vijijini. Mradi huu unatekelezwa kwa msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 1.70 bilioni zimepangwa kutumika.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kutoa mafunzo yakinifu ya vyanzo vya maji; na
ii. Kufanya upembuzi yakinifu juu ya vyanzo vya maji.

Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar

Programu ina lengo la kuimarisha huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo ya mijini na vijijini ili kuwawezesha wananchi kupata huduma hiyo kwa uhakika zaidi. Kwa mwaka 2022/23 programu imepangiwa jumla ya TZS 26.02 bilioni (TZS 14.73 bilioni kutoka Serikalini na TZS 11.29 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na imepanga kutekeleza miradi miwili ifuatayo:-

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme

Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha huduma salama na ya uhakika ya upatikanaji wa umeme katika maeneo ya mijini, vijijini na visiwa vidogo vidogo vya Zanzibar. Mradi huu

ni wa miaka minne (2021-2025) na unatarajiwa kugharimu jumla ya TZS 162.75 bilioni. Kwa mwaka 2022/23, Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 8.23 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kufanya utafiti wa uwekaji wa waya za umeme baharini ("submarine cable") mpya.

Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)

Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA) unatarajiwa kutekelezwa kwa miaka sita (2022-2027) na unakadiriwa kutumia jumla ya TZS 372.48 bilioni kwa lengo la kuimarisha utekelezaji katika sekta ya nishati kwa kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mshirika wa Maendeleo ambae ni Benki ya Dunia. Kwa mwaka 2022/23, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 17.79 bilioni (TZS 6.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 11.29 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha za Serikali

i. Ulipaji wa fidia katika maeneo yatakayoathirika na mradi.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa kwa Fedha Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

i. Kuajiri Washauri Elekezi wa kusimamia kazi ya uwekaji wa betri za kuhifadhia umeme wa jua, ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa jua na ujenzi wa njia kubwa ya umeme ya 132Kv;
ii. Kuajiri Wakandarasi kwa ajili ya kuanza kazi ya uwekaji wa betri za kuhifadhia umeme wa jua megawati 20, ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa jua na ujenzi wa njia kubwa ya umeme ya 132Kv;
iii. Kuajiri Mshauri Elekezi wa kazi ya usimamizi wa mfumo wa uunganishaji wa umeme "SCADA system";
iv. Kuajiri Mshauri Elekezi wa kuangalia masuala ya kijinsia katika sekta ya nishati; na
v. Kutoa elimu juu ya matumizi bora ya nishati kwa watumiaji.

9.16 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ina jukumu la kusimamia na kuendeleza masuala yote yanayohusiana na uchumi wa buluu Zanzibar ikiwemo utekelezaji wa shughuli za uvuvi wa bahari kuu, kilimo cha bahari, ufugaji wa mazao baharini, utalii wa baharini na fukwe, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia sambamba na uratibu wa utawala na mazingira ya baharini. Kwa mwaka 2022/23, Wizara imepanga kutekeleza jumla ya programu mbili na miradi minne ya maendeleo ambayo imepangiwa jumla ya TZS 81.55 bilioni ambapo TZS 52.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 29.55 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (TZS 2.3 bilioni ruzuku na TZS 27.25 bilioni ni mkopo).

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi

Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi imeanza mwaka 2021/22 ni ya miaka mitano (2021-2026) ambayo inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo ni kuongeza tija endelevu, uthabiti, faida na biashara ya mbegu za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki, kwa kutilia mkazo uwezeshaji wa wanawake na ushiriki wa vijana. Programu inatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo pekee. Kwa mwaka 2022/23, kiasi cha TZS 13.80 bilioni zinatarajiwa kutolewa.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kukamilisha tathmini ya athari za kimazingira kwa ajili ya ununuzi wa meli, ujenzi wa viwanda vya kusarifu samaki na vyumba vya baridi (Cold Storage);
ii. Kuanza utaratibu wa ununuzi wa meli za uvuvi na kuendeleza uvuvi wa bahari kuu;
iii. Kuanza ujenzi wa viwanda vya usarifu wa samaki na ujenzi wa vyumba vya baridi;
iv. Kuanza matayarisho ya mitambo ya kukaushia mazao ya baharini (mwani na majongoo);
v. Kutoa mafunzo kwa wakulima wa mwani na wafugaji wa majongoo ya pwani.

Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia

Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia ya juu na chini imeanza mwaka 2022/23 na inatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha

miaka mitano (2022-2027) kwa gharama ya jumla ya TZS 173.36 bilioni. Lengo kuu ni kuimarisha mnyororo wa thamani ya mafuta na gesi asilia kwa kutengeneza miundombinu inayotakikana. Programu hii itatekelezwa kupitia miradi mitatu na kwa mwaka 2022/23, imepangiwa jumla ya TZS 11.0 bilioni kutoka Serikali.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Utayarishaji wa upembuzi yakinifu, usarifu na michoro ya ujenzi;
ii. Kuanza ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhia na kusambazia gesi kwa wateja;
iii. Kuanza ujenzi wa matangi ya kuhifadhia mafuta (50,000MT);
iv. Ununuzi wa vifaa na uandaaji wa mifumo ya uhifadhi na usimamizi wa taarifa za mafuta na gesi asilia; na
v. Kutoa mafunzo kwa wataalamu kuhusu usimamizi wa taarifa za mafuta na gesi asilia.

Mradi wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu

Mradi wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu umeanzishwa kwa lengo la kuendeleza uvuvi mdogo mdogo na wa bahari kuu na ufugaji kwa maendeleo ya uchumi wa buluu. Mradi huu wa miaka mitano (2022-2027) utatekelezwa kwa fedha za Mshirika wa Maendeleo ambae ni Benki ya Dunia na unatarajia kuanza 2022/23. Kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 13.45 bilioni zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari;
ii. Kuimarisha mfumo wa taarifa za pwani na bahari;
iii. Ununuzi wa vifaa vya mawasiliano;
iv. Ujenzi wa majengo ya uhifadhi na utafiti; na
v. Kuandaa na kupitia sera, sheria na kanuni.

Mradi wa Uanzishwaji wa Viwanda vya Maboti na Kusarifu Samaki na Dagaa

Mradi wa Uanzishwaji wa Viwanda vya Maboti na Kusarifu Samaki na Dagaa ni wa miaka miwili (2022-2024) na umeanza mwa 2022/23. Lengo la mradi huu ni kuongeza ubora wa samaki na bidhaa za samaki pamoja na

kupunguza upotevu wa ubora wa bidhaa. Mradi huu unatarajiwa kuwa ni wa mashirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi. Kwa mwaka 2022/23, jumla ya TZS 11.0 bilioni kutoka katika fedha za maendeleo za Serikali zimepangwa kutumika.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa viwanda vya maboti;
ii. Ujenzi wa kiwanda cha chakula cha samaki; na
iii. Ujenzi wa viwanda vya barafu na hifadhi ya samaki.

Mradi wa Ujenzi wa Bandari za Uvuvi

Mradi wa Ujenzi wa Bandari za Kisasa za Uvuvi ni wa miaka minne 2022-2026 kwa lengo kuu la mradi huu ni kuwawezesha wavuvi kuweza kupata huduma za msingi kwa kurahisisha uwepo wa masoko na bandari za uvuvi. Mradi unatarajiwa kugharimu jumla ya TZS 90.0 bilioni na umepangwa kujenga bandari sita za uvuvi katika maeneo ya Kizimkazi, Mkokotoni na Nungwi kwa Unguja na Shumba Mjini, Wete na Mkoani kwa Pemba. Kwa mwaka 2022/23 mradi umepangwa kuanza ujenzi wa bandari mbili na umepangiwa kiasi cha TZS 30.0 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Shumba Mjini na Kizimkazi.

Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini

Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini umeanza mwaka 2022/23 na unatarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitano (2022-2027). Lengo kuu la mradi ni kuwawezesha wakulima na wasindikaji wa mazao ya baharini kufikia maendeleo endelevu ya mnyororo wa thamani. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Mshirika wa Maendeleo peke yake ambapo kwa mwaka 2022/23 umepangiwa kiasi cha TZS 2.3 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kuanzisha mashamba nane ya majaribio ya mwani/majongoo bahari;
ii. Kuanzisha vitalu vinne vya mwani na majongoo bahari;
iii. Kutoa mafunzo kwa wanawake 8,000 ambao ni wakulima wa majongoo bahari;
iv. Kutoa mafunzo kwa maafisa ugani 10 na watafiti 20 wa taasisi za umma; na

v. Kuwapatia vifaa na nyenzo wakulima wa mwani na wafugaji majongoo bahari.

9.17 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

Wizara hii inajumusiha sekta kuu tatu ambazo ni ujenzi, mawasiliano na uchukuzi. Sekta hizi ni miongoni mwa sekta kuu zinazoharakisha maendeleo ya sekta nyengine na ukuaji wa uchumi wa Taifa. Kwa mwaka 2022/23, Wizara imepangiwa kutumia jumla ya TZS 564.01 bilioni (TZS 226.15 bilioni kutoka Serikalini na TZS 337.86 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa utekelezaji wa programu nne na mradi mmoja wa maendeleo.

Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu

Programu hii ina lengo la kujenga barabara kwa kiwango cha lami, ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa taa na alama za barabarani kwa barabara kuu za Unguja na Pemba. Ukamilikaji wa barabara hizi utasaidia kuhuisha uchumi na uwekezaji kwa vile barabara hizi ni kiunganishi cha miji na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari. Programu hii inatarajiwa kuanza utekelezaji wake mwaka wa fedha 2022/23, na itahusisha ujenzi wa barabara kuu mbalimbali ikiwemo barabara mpya na zinazoendelea, inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa jumla ya TZS 249.71 bilioni (TZS 37.95 bilioni kutoka Serikalini na TZS 211.76 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali

i. Ulipaji wa fidia kwa vipando na nyumba zitakazoathirika na ujenzi wa barabara ya Wete – Chake Chake km 22, Fumba – Kisauni km 12 na Chake Chake – Mkoani km 43; na Tunguu Makunduchi km 48.5.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na na Washirika wa Maendeleo

i. Kuanza ujenzi wa barabara kwa uwekaji fusi na kitanda cha barabara pamoja na matabaka ya lami kwa barabara ya Chake Chake – Wete km 22;

ii. Kuanza kazi ya ujenzi kwa uwekaji wa kitanda, fusi pamoja na ujenzi wa madaraja na makalavati kwa barabara ya Chake Chake -Mkoani km 43;

iii. Kuendelea na uwekaji wa kifusi tabaka la kwanza pamoja na ujenzi

wa makalavati kwa baadhi ya maeneo katika barabara ya Tunguu - Makunduchi km 48.5; na

iv. Upimaji na usafishaji wa eneo la barabara, ujenzi wa matabaka ya barabara pamoja na uwekaji wa lami kwa barabara ya Fumba-Kisauni km 12.

Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani

Programu hii itahusisha ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo mbalimbali ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Programu imeanza mwaka 2021/22, kukamilika kwa barabara hizi kutasaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuunganisha vijiji na mitaa mbalimbali na barabara kuu na kupendezesha haiba sambamba na kuchochea huduma za usafirishaji wa watu na mzigo na kuchochea ukuaji wa uchumi na kuimarika kwa sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo sekta ya kilimo na biashara. Kwa mwaka 2022/23, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 30.0 bilioni.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kufanya tathmini ya ujenzi na ulipaji wa fidia kwa baadhi ya barabara za ndani;

ii. Usafishaji wa maeneo pamoja na kuanza uwekaji wa fusi na lami kwa baadhi ya barabara;

iii. Ujenzi wa mitaro pamoja na uwekaji wa lami kwa baadhi ya barabara ambazo zimeshaanza; na

iv. Uwekaji wa alama na taa za barabarani kwa barabara zilizokamilika.

Programu ya Matengenezo ya barabara za Mjini

Programu hii itahusisha uimarishaji wa kilomita 103.7 za barabara za miji, kwa mwaka 2022/23 programu inalenga kujenga barabara za Mkoa wa Mjini Magharibi. Aidha, itahusisha ujenzi wa barabara kuu, njia za wapita kwa miguu, uwekaji wa taa na ujenzi wa mitaro ya maji. Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kupendezesha haiba ya miji yetu na kuimarika kwa sekta ya usafirishaji, biashara na utalii. Kwa mwaka 2022/23 programu imepangiwa jumla ya TZS 135.6 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Ujenzi wa miundombinu yaa barabara kuu za njia mbili (Two lanes dual) ikiwemo Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume – Kiinua Miguu (5.2 km), Kiembesamaki-Amani-Mtoni (Mkapa road) (km 8.8), Kariakoo – Magomeni-Mwanakwerekwe Sokoni (km 2.9), Kinazini (BOT) - Mtoni (km 3.5) Amani Round about-Mikunguni-Kwabiziredi (km 2.6);

ii. Ujenzi wa mindombinu kwa barabara kuu za njia moja (single carriage way) ikiwemo barabara ya Mazizini –ZRB- Mombasa na kituo cha polisi Ng'ambo – Mfereji wa Wima;

iii. Kufanya ukarabati wa barabara ndogo ndogo ikiwemo barabara ya Mazizini kituo cha Polisi - Chukwani Jeshini, Mazizini – Vitambulisho - Soko la samaki, Mazizini VP2-Migombani, Miembeni round about –Michenzani jumba namba moja na tisa, Miembeni round about – Bomani- Hospitali ya Kidongo Chekundu, Saateni - Kwalimsha- JKU, Jangombe - Matarumbeta, Gulioni Gapco – Makadara -Kwa Abass Hussein, Kijangwani Posta-hospitali ya Mwembeladu – Miti Ulaya, Mtendeni - Michenzani, Michenzani Jumba nambari 10 – Gongoni – Kisiwandui - Msikiti Mabati, Skuli ya Kisiwandui - Mskiti Mabati - CRDB – Maisara - Welles – Skuli ya Haile Selassie, Skuli ya Benbella -Kikwajuni/ Maisara - Kikwajuni Mau - Michenzani, Kinazini- skuli ya Lumumba -Zanroad-Lumumba ZECO – Saateni, Mtoni depot-ZECO power station - Mtoni Kidatu, Mwembe Makumbi - Karakana – Basra – Skuli ya Mtopepo;

iv. Kuanza ujenzi kwa barabara ndogo zisizo na lami ikiwemo barabara ya Rahaleo ZBC-Bizredi – Michenzani, Mpendae, Chukwani mwisho - Buyu, Kilimani Bar - Jangombe, Kwakira - Kituo kipya uwanja wa ndege, Mbweni afya – Madina - Mbweni Matrekta, ZSSF Mbweni Estate - Mbweni ruins - Mbweni BOT quater - Kiembesamaki, Baraza la Wawakilishi Chukwani - Makamo wa Kwanza wa Rais, River tiba –Chukwani tuta, Faraja Skuli - Mboriborini, Masumbani tawi la Kilimahewa - Shaurimoyo skuli, Saateni JKU - Reserved Storage - Saaten tangi la maji/Shaurimoyo skuli, Makadara mfereji wa Wima & Associate, Darajabovu Mboriborini, Magazeti Press-Mkele, Msikiti Shurba-Mshelishelini - Matarumbeta, Muungano Mwembe Mkali, Muungano - Sogea, Mnara wa mbao - Migombani Garden; na

v. Kuzifanyia matengenezo “round about” ya Mwanakwerekwe na Amani.

Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege

Programu ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa na viwango vya kimataifa, programu ilianzishwa mwaka 2011/21 inahusisha uimarishaji wa viwanja vya ndege ikiwemo maegesho, njia za kupitia ndege pamoja na sehemu za kukaa abiria. Programu inatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa jumla ya TZS 140.7 bilioni (TZS 14.6 bilioni kutoka Serikalini na TZS 126.1 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Serikali

i. Kuendelea na ujenzi wa uwanja mdogo wa Kigunda kwa uimarishaji njia ya kutulia ndege na sehemu za abiria; na

ii. Ulipaji wa fidia kwa ujenzi wa uwanja wa ndege Pemba.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa na Washirika wa Maendeleo

i. Usafishaji wa eneo pamoja na kuanza kwa ujenzi wa uwanja wa ndege Pemba.

Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani

Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani utajumuisha bandari ya mizigo, mafuta na gesi na chelezo. Mradi una lengo la kusaidia shughuli za usafirishaji wa bidhaa na mizigo na kusaidia maendeleo ya sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo sekta ya biashara na sekta ya viwanda. Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali na Wawekezaji kutoka katika sekta binafsi. Kwa mwaka 2022/23 mradi umepangiwa jumla ya TZS 8.0 bilioni kutoka Serikalini.

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Upelekaji wa miundombinu ya maji, umeme na barabara katika eneo la ujenzi wa bandari; na

ii. Kufanya uratibu na usimamizi wa mradi.

9.18 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

Wizara ina jukumu la kusimamia utalii na mambo ya kale kwa kuongeza vivutio vipya sambamba na kuitangaza Zanzibar kiutalii. Kwa mwaka 2022/23, Wizara hii inatarajia kutekeleza programu moja ya maendeleo yenye jumla ya TZS 7.50 bilioni kutoka Serikalini itakayosaidia kuleta mageuzi katika sekta ya utalii na mambo ya kale.

Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria

Sekta ya Utalii ni sekta ya huduma inayokua kwa kasi hapa Zanzibar ambapo hutoa fursa nyingi za ajira na kuongeza Pato la Taifa. Programu ilianza mwaka 2017/18 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2024/25. Kwa mwaka 2022/23, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 7.50 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Shughuli Zilizopangwa Kutekelezwa

i. Kufanya matengenezo ya nyumba ya ASP Kijangwani;
ii. Matengenezo ya nyumba ya wahindi Fufuni Pemba;
iii. Matengenezo ya msikiti wa Kichokochwe Pemba;
iv. Kuimarisha eneo la Ras Mkumbuu;
v. Kuimarisha maeneo ya kihistoria ya Maruhubi - Unguja na Makangale - Pemba;
vi. Kuimarisha eneo la kihistoria la Mkamandume awamu ya Pili; na
vii. Kuimarisha eneo la kihistoria la Fukuchani (Mvuleni) awamu ya pili.

10. PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA MFUKO WA MIUNDOMBINU (INFRASTRUCTURE FUND)

Mfuko wa Miundombinu (Infrastructure Fund) ni mfuko maalum ulioanzishwa mwaka 2015 chini ya kifungu nambari 11 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2005 kwa ajili ya kusaidia uimarishaji wa miundombinu. Mfuko huu ulianza kazi zake rasmi tarehe 1 Julai 2015 na unalenga kukusanya rasilimali kutoka katika kodi za miundombinu na katika vyanzo vyengine kwa lengo la kusaidia maendeleo ya Zanzibar. Aidha, rasilimali za Mfuko huu zinatolewa kwa lengo kuu la kuwekeza katika miundombinu ya umma ili kusaidia kunyanyua uchumi na maendeleo ya jamii.

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo unaendelea kupata fungu kutoka Mfuko huu ambapo mwaka 2022/23 jumla ya TZS 28.60 bilioni zimepangwa

kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa shughuli za programu na miradi mbali mbali ya maendeleo. Programu moja na miradi miwili ya maendeleo imepangwa kutekelezwa kupitia Mfuko wa Miundombinu.

*i. **Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege***;
   a) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba,
   b) Ujenzi wa Uwanja Mdogo wa Kigunda,

*ii. **Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi – Mangapwani;***

*iii. **Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati.***

Mchanganuo wa mgawanyo wa fedha zilizopangwa kwa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo itayopatiwa fedha kupitia Mfuko wa Miundombinu Kiwizara unaonekana katika Kiambatisho nambari 2.

11.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI

Kwa mwaka 2022/23, Serikali kupitia Tume ya Mipango Zanzibar imepanga kusimamia kwa karibu masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo kupitia maeneo yafuatayo:-

i. Kuandaa muongozo wa utekelezaji wa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini;

ii. Kushirikiana na sekta katika kutekeleza Mfumo wa kidigitali wa Ufuatiliaji na Tathmini (Digital M & E System) kwa program na miradi ya maendeleo ili kuleta matokeo kwa malengo makuu (goals), matokeo ya muda wa kati (outcome), na muda mfupi (output), shabaha (targets) na viashiria vitakavyotumika kupima matokeo hayo;

iii. Kufanya ufuatiliaji kwa programu na miradi yote ya maendeleo itakayoingiziwa fedha na kufanya tathmini kwa program na miradi itakayokamilika.

12.0 WASHIRIKA WA MAENDELEO

Washirika wa Maendeleo watakaochangia bajeti ya programu na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na Adaptation Fund (AF), AfDB, AMREF, BADEA, Basket Fund (BF), Benki ya Dunia, EXIM BANK (INDIA), GEF, Germany, Global Fund (GF), Good Neighbour, GPE, IAEA, IFAD, Khalifa Fund, KOICA, KOREA, MILELE FOUNDATION,

NORWAY, OMAN, SAUDI FUND (SF), SIDA -DLI, TfT, UAE, UNDP, UNEP, UNFPA, UNESCO, UNICEF, USDA-USAID na UN-WOMEN.

13.0 HITIMISHO

Utayarishaji wa Kitabu cha Pili cha Mwelekeo wa hali ya uchumi mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo 2022/23 umeshirikisha wadau mbali mbali wakiwemo Wizara, Taasisi za Serikali, Washirika wa Maendeleo na Asasi za Kiraia. Hivyo, kazi zilizoainishwa ndani ya kitabu hiki zinatarajiwa kutekelezwa na wahusika wote ili kuweza kupata mafanikio ya kukuza uchumi na kuondoa changamoto za maendeleo ikiwa ni hatua ya kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Dira ya Maendeleo ya 2050 na kufanikisha Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) na Malengo Endelevu ya Dunia (SDG's).

Matarajio ni kuwa Wizara, Taasisi na Idara za Serikali watakitumia kitabu hiki kwa madhumuni ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa programu na miradi iliyoainishwa. Aidha, Wizara zitatakiwa kutayarisha utekelezaji wa malengo kwa kila robo mwaka kwa kutumia taarifa zitazotokana na shughuli zilizomo ndani ya kitabu hiki. Taarifa za utekelezaji zitahitajika kuwasilishwa Tume ikiwemo utekelezaji halisi na kifedha kila baada ya wiki ya pili ya robo ya mwaka kukamilika.

Tume ya Mipango pia inaomba Wizara na Taasisi kuendelea na utaratibu wa kutayarisha na kuwasilisha Tume mtiririko wa fedha (Cash Flow) za programu na miradi katikati ya mwezi wa Julai 2022 sambamba na kuwasilisha maombi ya fedha za utekelezaji wa shughuli za programu/mradi kila wiki ya mwanzo ya mwezi husika ikifuatana na utekelezaji wa kipindi kilichopita. Inasisitizwa kuwa uwasilishaji wa maombi ya fedha uambatanishwe na vielelezo stahiki kwa mujibu wa shughuli za programu au mradi kama ilivyokubalika Serikalini ikiwemo mikataba. Mashirikiano makubwa yanahitajika kwa Wizara na Taasisi za Serikali katika kufanikisha malengo yetu.

Kurasa zifuatazo zina viambatisho ambavyo vinaonesha mgawanyo wa fedha za Programu na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2022/23. Mgawanyo wa fedha za SMZ na Washirika wa Maendeleo kwa programu na miradi ya maendeleo Kiwizara unaonekana katika kiambatisho namba 1.

VIAMBATANISHO

Kiambatisho Nam 1: PROGRAMU/MIRADI INAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA NA SERIKALI NA WASHIRIKA WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022/2023

KIFUNGU	PROGRAMU/MIRADI	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2021/22 ("000")	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/23 ("000")	MICHANGO YA WAHISANI ("000")			JUMLA YA BAJETI
				MUHISANI	RUZUKU	MKOPO	
A01	**OFISI YA RAIS - IKULU**						
	i) Mradi wa Uimarishaji wa Nyumba za Viongozi na Nyumba za Serikali	5,500,000	2,400,000				2,400,000
	ii) Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais		1,600,000				1,600,000
	JUMLA YA FUNGU	**6,000,000**	**4,000,000**		**-**	**-**	**4,000,000**
A07	**OFISI YA RAIS - KAZI NA UWEZESHAJI**						
	Programu ya Kuimarisha Uwezeshaji Wananchi Zanzibar	5,500,000	27,600,000				27,600,000
	JUMLA YA FUNGU	**6,465,000**	**27,600,000**		**-**	**-**	**27,600,000**
A08	**OFISI YA RAIS - UCHUMI NA UWEKEZAJI**						
	Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji	8,500,000	15,100,000				15,100,000
	JUMLA YA FUNGU	**8,500,000**	**15,100,000**	**-**	**-**	**-**	**15,100,000**
F01	**OFISI YA RAIS - FEDHA NA MIPANGO**						
	Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar	76,379,478	92,200,000				92,200,000
	Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)			BENKI YA DUNIA		47,131,600	47,131,600
	Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP)			NORWAY	2,661,058		2,661,058
	Mradi						
	i) Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili			AfDB		1,460,358	1,460,358
	JUMLA YA FUNGU	**76,379,478**	**92,200,000**		**2,661,058**	**48,591,958**	**143,453,017**

KIFUNGU	PROGRAMU/MIRADI	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2021/22 ("000")	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/23 ("000")	MICHANGO YA WAHISANI ("000")			JUMLA YA BAJETI
				MUHISANI	RUZUKU	MKOPO	
F03	**TUME YA MIPANGO**						
	Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)	2,000,000	4,000,000	URT	500,000		4,500,000
	Miradi						
	i) Usimamizi, Kujenga Uwezo na Kuoanisha Mipango ya Kisekta, Kitaifa na Kimataifa (ZADEP, SDGs na African Agenda)		300,000	UNDP	230,000		530,000
	ii) Uratibu wa Shughuli za Kupambana na Umasikini		800,000				800,000
	iii) Usimamizi wa Upembuzi Yakinifu wa Programu na Miradi		6,988,539				6,988,539
	JUMLA YA FUNGU	**2,000,000**	**12,088,539**		**730,000**	**-**	**12,818,539**
F04	**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**						
	i) Mradi wa Uendelezaji Takwimu		500,000	UNICEF/USAID/UNFPA/BF/ UN WOMEN	8,396,496	4,370,000	13,266,496
	JUMLA YA FUNGU	**-**	**500,000**		**8,396,496**	**4,370,000**	**13,266,496**
G01	**OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**						
	Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (Phase II)	1,199,875	528,155				528,155
	Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria	531,300	1,152,000				1,152,000
	JUMLA YA FUNGU	**1,731,175**	**1,680,155**		**-**	**-**	**1,680,155**
G02	**MAHKAMA KUU**						
	i) Mradi wa Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi *(ECMIS)*		1,000,000				1,000,000

KIFUNGU	PROGRAMU/MIRADI	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2021/22 ("000")	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/23 ("000")	MICHANGO YA WAHISANI ("000")			JUMLA YA BAJETI
				MUHISANI	RUZUKU	MKOPO	
	ii) Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Mikoa		5,550,000				5,550,000
	JUMLA YA FUNGU		**6,550,000**		**-**		**6,550,000**
D01	**AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ**						
	ii) Mradi wa Zanzibar Salama	12,000,000	7,400,000				7,400,000
	iii) Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Taka na Maji Taka Zanzibar		7,800,000				7,800,000
	iv) Mradi wa Kuimarisha Uzalishaji wa Idara Maalum za SMZ		3,720,000				3,720,000
	JUMLA YA FUNGU	**17,900,978**	**18,920,000**		**-**	**-**	**18,920,000**
D12	**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR**						
	Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili	1,000,000	1,100,000				1,100,000
	JUMLA YA FUNGU	**1,000,000**	**1,100,000**		**-**	**-**	**1,100,000**
D04	**KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO**						
	i) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM	4,264,000	3,000,000				3,000,000
	ii) Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Uzamiaji na Uokozi	62,192,364	2,100,000				2,100,000
	iii) Mradi wa Uwekaji wa Rada		9,320,000				9,320,000
	JUMLA YA FUNGU	**66,456,364**	**14,420,000**		**-**	**-**	**14,420,000**
D06	**KIKOSI CHA VALANTIA**						
	Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Mahanga ya KVZ	4,170,000	3,170,000				3,170,000
	JUMLA YA FUNGU	**4,170,000**	**3,170,000**		**-**	**-**	**3,170,000**
D03	**CHUO CHA MAFUNZO**						
	Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga - Chuo Cha Mafunzo	3,232,650	2,232,650				2,232,650
	JUMLA YA FUNGU	**3,232,650**	**2,232,650**		**-**	**-**	**2,232,650**

KIFUNGU	PROGRAMU/MIRADI	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2021/22 ("000")	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/23 ("000")	MICHANGO YA WAHISANI ("000")			JUMLA YA BAJETI
				MUHISANI	RUZUKU	MKOPO	
D02	**JESHI LA KUJENGA UCHUMI**						
	i) Mradi wa Ujenzi waNyumba na Mahanga ya Kambi za JKU	4,161,197	3,250,000				3,250,000
	iii) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Wakala wa JKU		2,214,765				2,214,765
	JUMLA YA FUNGU	**10,814,623**	**5,464,765**	**-**	**-**	**-**	**5,464,765**
D05	**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI**						
	i) Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari - KZU	5,206,894	4,000,000				4,000,000
	ii) Mradi wa Ununuzi wa Magari ya Zimamoto		2,000,000				2,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**5,206,894**	**6,000,000**		**-**	**-**	**6,000,000**
B01	**OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS**						
	i) Mradi wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira	300,000	4,500,000				4,500,000
	ii) Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi wa Jamii ya Pwani			AF	796,030		796,030
	iii) Mradi wa Uhimili wa Mabadiliko wa Tabianchi kwa kutumia Mfumo Ikolojia Vijijini			UNEP	318,617		318,617
	JUMLA YA FUNGU	**300,000**	**4,500,000**		**1,114,647**	**-**	**5,614,647**
	MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA MADAWA YA KULEVYA						
	Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Madawa ya Kulevya	1,900,000	3,637,825				3,637,825
	JUMLA YA FUNGU	**1,900,000**	**3,637,825**		**-**	**-**	**3,637,825**
C01	**OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI**						
	Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III)	100,000	100,000	BENKI YA DUNIA		14,644,434	14,744,434
	JUMLA YA FUNGU	**100,000**	**100,000**		**-**	**14,644,434**	**14,744,434**

KIFUNGU	PROGRAMU/MIRADI	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2021/22 ("000")	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/23 ("000")	MICHANGO YA WAHISANI ("000")			JUMLA YA BAJETI
				MUHISANI	RUZUKU	MKOPO	
H03	**WIZARA YA AFYA**						
	Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar	713,545	513,352	AMREF/GF	3,422,422		3,935,774
	Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto	1,000,000	1,517,588	UNFPA	1,715,978		3,233,566
	Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma	1,000,000	94,288	GF	4,944,315		5,038,603
	Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya						
	i) Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa Unguja	3,000,000	3,500,000				3,500,000
	ii) Ujenzi wa Maabara ya Wakala wa Chakula na Dawa - Unguja	2,000,000	4,469,567				4,469,567
	iii) Kuzipandisha Hadhi Hospitali za Wilaya na Hospitali za Vijiji	8,000,000	8,950,107				8,950,107
	iv) Ujenzi wa Hospital ya Mahonda			OMAN	11,500,000		11,500,000
	v) Ujenzi wa Maabara ya Biochemistry Binguni	1,500,000	4,500,000				4,500,000
	vi) Ujenzi wa Hospital ya Wete	100,000	100,000	UAE	3,648,000		3,748,000
	Miradi						
	i) Kuanzisha Bima ya Afya Zanzibar		1,549,893				1,549,893
	ii) Kuwekeza katika Huduma za Mama na Mtoto			WB		10,300,000	10,300,000
	JUMLA YA FUNGU	**72,313,545**	**25,194,795**		**25,230,714**	**10,300,000**	**60,725,509**
H01	**HOSPITALI YA MNAZI MMOJA**						
	Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja	10,279,946	5,553,000	BADEA		7,969,219	13,522,219
	JUMLA YA FUNGU	**10,279,946**	**5,553,000**		**-**	**7,969,219**	**13,522,219**

KIFUNGU	PROGRAMU/MIRADI	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2021/22 ("000")	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/23 ("000")	MICHANGO YA WAHISANI ("000")			JUMLA YA BAJETI
				MUHISANI	RUZUKU	MKOPO	
N02	**WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**						
	i) Mradi wa Matengenezo ya Nyumba za Maendeleo		*16,000,000*				*16,000,000*
	ii) Mradi wa Utayarishaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi		*1,000,000*				*1,000,000*
	JUMLA YA FUNGU	**10,310,000**	**17,000,000**		**-**	**-**	**17,000,000**
R01	**WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA**						
	Programu ya Kuendeleza Viwanda						
	i) Kuanzisha na kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks)	2,776,000	2,500,000				2,500,000
	ii) Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa	4,500,000	4,500,000	KHALIFA FUND	4,600,000		9,100,000
	Mradi						
	i) Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar	4,000,000	4,000,000				4,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**11,276,000**	**11,000,000**		**4,600,000**	**-**	**15,600,000**
K01	**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**						
	i) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi	4,330,040	10,496,239	SIDA/TFT/ GPE/KOICA /UNICEF	10,463,474		20,959,713
	ii) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima	850,000	21,978,260	WB/GPE/ SIDA/KOICA/ BADEA/ KOREA	5,202,900	16,335,000	43,516,160
	iii) Mradi wa Kuimarisha Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali	6,220,667	4,500,000	AfDB		28,750,000	33,250,000
	JUMLA YA FUNGU	**45,583,387**	**36,974,499**		**15,666,374**	**45,085,000**	**97,725,873**

KIFUNGU	PROGRAMU/MIRADI	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2021/22 ("000")	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/23 ("000")	MICHANGO YA WAHISANI ("000")			JUMLA YA BAJETI
				MUHISANI	RUZUKU	MKOPO	
J03	**WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO**						
	Programu ya Ajira kwa Vijana	7,000,000	6,400,000				6,400,000
	Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo						
	i) Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya	4,000,000	4,000,000				4,000,000
	ii) Ujenzi wa Viwanja na Vyuo vya Michezo	3,000,000	3,000,000				3,000,000
	Programu ya Uimarishaji wa Utoaji wa Matangazo (ZBC)		12,337,261				12,337,261
	Miradi						
	i) Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa		5,000,000				5,000,000
	ii) Uendelezaji wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji	9,520,000	2,000,000				2,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**37,267,481**	**32,737,261**		**-**	**-**	**32,737,261**
L01	**WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO**						
	Programu ya Umwagiliaji	2,900,000	500,000	KOREA		20,000,000	20,500,000
	Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo						
	i) Kurejesha Urithi wa Kijani		1,000,000				1,000,000
	ii) Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo	1,700,000	5,000,000				5,000,000
	Programu ya Kudhibiti Maradhi na Upotevu wa Mazao	120,000					
	i) Kupambana na Sumukuvu Tanzania (TANIPAC)			AfDB		1,259,000	1,259,000
	ii) Kudhibiti Upotevu wa Mazao	120,000	2,194,847	IAEA	388,240		2,583,087
	JUMLA YA FUNGU	**4,840,000**	**8,694,847**		**388,240**	**21,259,000**	**30,342,087**

KIFUNGU	PROGRAMU/MIRADI	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2021/22 ("000")	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/23 ("000")	MICHANGO YA WAHISANI ("000")			JUMLA YA BAJETI
				MUHISANI	RUZUKU	MKOPO	
H03	**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,WAZEE NA WATOTO**						
	Mradi wa Hifadhi ya Wazee	3,900,000	3,000,000				3,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**3,900,000**	**3,000,000**		**-**	**-**	**3,000,000**
N03	**WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI**						
	Program ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar						
	i) Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA)	600,000	3,500,000	INDIA (EXIM BANK)		66,855,577	70,355,577
	ii) Uendelezaji wa Visima vya Ras el Khaimah	8,052,284	18,154,964				18,154,964
	iii) Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar		1,090,700	INDIA (EXIM BANK)		11,385,000	12,475,700
	iv) Uimarishaji wa Huduma za Maji Zanzibar			KFW/ Germany	1,700,000		1,700,000
	Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar						
	ii) Kuimarisha Miundombinu ya Umeme	2,000,000	8,229,000				8,229,000
	iii) Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)	1,500,000	6,500,000	BENKI YA DUNIA		11,289,780	17,789,780
	JUMLA YA FUNGU	**14,152,284**	**37,474,664**		**1,700,000**	**89,530,357**	**128,705,021**
L02	**WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**						
	Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi			IFAD		13,800,000	13,800,000
	Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia		*11,000,000*				*11,000,000*
	Miradi						

KIFUNGU	PROGRAMU/MIRADI	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2021/22 ("000")	MAKISIO YA SMZ KWA MWAKA 2022/23 ("000")	MICHANGO YA WAHISANI ("000")			JUMLA YA BAJETI
				MUHISANI	RUZUKU	MKOPO	
	i) Uanzishwaji wa Viwanda vya Maboti na Kusarifu Samaki na Dagaa	4,277,607	11,000,000				11,000,000
	ii) Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini			*KOICA*	*2,300,000*		*2,300,000*
	iii) Ujenzi wa Bandari za Kisasa za Uvuvi		*30,000,000*				*30,000,000*
	iv) Mradi wa Maendeleo ya Uchumi wa Buluu			*WB*		*13,455,000*	*13,455,000*
	JUMLA YA FUNGU	**16,633,600**	**52,000,000**		**2,300,000**	**27,255,000**	**81,555,000**
P01	**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**						
	Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu		37,947,000	BADEA/SF		211,760,000	249,707,000
	Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani		*30,000,000*				*30,000,000*
	Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini		*135,600,000*				*135,600,000*
	Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege						
	i) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba	2,000,000	8,000,000			126,100,000	134,100,000
	ii) Ujenzi wa Uwanja Mdogo wa Kigunda	8,000,000	6,600,000				6,600,000
	Miradi						
	i) Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani	3,000,000	8,000,000				8,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**115,991,000**	**226,147,000**		**-**	**337,860,000**	**564,007,000**
J01	**WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE**						
	Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria	3,500,000	7,500,000				7,500,000
	JUMLA YA FUNGU	**3,500,000**	**7,500,000**		**-**	**-**	**7,500,000**
	JUMLA YA KUBWA	**606,500,000**	**682,540,000**		**62,787,529**	**606,864,969**	**1,352,192,497**
	JUMLA YA FEDHA ZA WAHISANI					**669,652,497**	

Kiambatisho namba 2:

PROGRAMU/MIRADI INAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA NA SERIKALI KUPITIA MFUKO WA MIUNDOMBINU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2022/2023		
KIFUNGU	**PROGRAMU/MIRADI**	**MAKISIO SMZ 2022/23 ("000")**
P01	**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**	
	Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege	
	i) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba	8,000,000
	ii) Ujenzi wa Uwanja Mdogo wa Kigunda	6,600,000
	Mradi	
	i) Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani	8,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**22,600,000**
N03	**WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI**	
	i) Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati	6,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**6,000,000**
	JUMLA YA KUBWA	**28,600,000**